# TAFSIRI YA SUURAT YUUNUS

## UTANGULIZI

Makala hizi zimekusanywa kutoka radio ya kiswahili ya iran, na lengo hasa la kuzikusanya makala hizi, ni kueneza na kusambaza utamaduni wa kiislamu ulimwenguni. kwa hiyo basi ukusanyaji huu haukulenga malengo ya aina yeyote isipokua ni kama ilivyotajwa hapo juu.


## MKUSANYAJI WA MAKALA HIZI NI:

## SALIM SAID AL-RAJIHIY

1

# TAFSIRI YA SUURAT YUUNUS

## MWANZO WA MAKALA

Bismillahir Rahmanir Rahim.

Ifuatayo ni tarjumi na maelezo mafupimafupi ya Sura ya 10 ya Qur'ani Tukufu ambayo inaitwa Surat Yunus.

Jina la sura hii linatokana na jina la Nabii Yunus (a.s), ambaye ni Mtume wa Mwenyezi Mungu aliyekuja baada ya Manabii: Nuh na Musa (a.s).

### AYA YA KWANZA NA YA PILI

Tunaianza basi darsa letu hili kwa aya ya kwanza na ya pili za sura hiyo ambazo zinasema:

الر تِلْكَ آيَاتُ الْكِتَابِ الْحَكِيمِ ﴿١﴾

1. Alif lam Ra. Hizi ni aya za kitab chenye hikima.

أَكَانَ لِلنَّاسِ عَجَبًا أَنْ أَوْحَيْنَا إِلَىٰ رَجُلٍ مِّنْهُمْ أَنْ أَنذِرِ النَّاسَ وَبَشِّرِ الَّذِينَ آمَنُوا أَنَّ لَهُمْ قَدَمَ
صِدْقٍ عِندَ رَبِّهِمْ قَالَ الْكَافِرُونَ إِنَّ هَٰذَا لَسَاحِرٌ مُّبِينٌ ﴿٢﴾

2. Je ni ajabu kwa watu ya kwamba tumemfunulia wahyi mtu miongoni mwao kuwa: Waonye watu na wape walioamini habari njema ya kwamba watakuwa na cheo kikubwa mbele ya Mola wao?. Wakasema makafiri: "Hayakuwa haya ila ni kiini macho.

Kama tulivyowahi kueleza wakati tulipoizungumzia sura ya pili ya al Baqarah, ni kwamba kati ya sura zote 114 za quran tukufu, sura 29 kati yao zinaanza kwa herufi za mkato kama alif lam mim, hamim, yasin n.k. Na tukasema kuwa kwa kuwa aya zinazofuatia baada ya aya hizo mara nyingi huzungumzia adhama ya quran, baadhi ya wafasiri wanasema lengo lililokusudiwa katika kutanguliza aya hizo ni kutolewa changamoto kwa wasioiamini quran, kwa maana kwamba Mwenyezi Mungu ameteremsha quran kwa kutumia herufi hizo, hivyo nanyi pia kama mnao uwezo teremsheni quran mfano wa hiyo.

Mojawapo ya sifa ambazo Mwenyezi Mungu ameitaja kuwa kimepambika nayo kitabu chake kitukufu cha quran ni hikima. Na hii ni kwa sababu hukumu za dini zilizokuja ndani ya kitabu hicho zimesimama juu ya hoja madhubuti na yale yaliyomo ndani yake ni mafunzo yenye hekima kubwa.

Baada ya kueleza hadhi na nafasi ya quran, katika aya ya pili Mwenyezi Mungu anabainisha nafasi na hadhi ya Mtume wake na kueleza kuwa watu wanatarajia kuona Mwenyezi Mungu akiteremsha Malaika kwa ajili ya kuwafikisha wao uongofu ,wakati kwa kuwa wao ni wanaadamu akili inahukumu kwamba Mtume atakayetumwa kwao lazima naye awe ni mtu kama wao, na anayezungumza lugha yao ili matendo na mwenendo wake wa maisha uweze kuwa kigezo kwao.

Kazi ya Mitume hao ni kutoa bishara njema kwa wafanyao mema na kuwaonya wale watendao mabaya. Lakini kutokana na baadhi ya wakati kuonyesha miujiza ya kuthibitisha ukweli wa unabii wao, baadhi ya watu wasiokuwa tayari kuiamini haki huwasingizia Mitume hao kuwa ni wachawi. Miongoni mwa mafunzo tunayoyapata kutokana na aya hizi ni

kuwa quran ni kitabu imara na cha milele, kiasi kwamba kupita kwa wakati hakuwezi kupunguza hata chembe thamani na itibari ya kitabu hicho.

### AYA YA TATU

Ifuatayo sasa ni aya ya 3 ya sura hiyo ambayo inasema:

إِنَّ رَبَّكُمُ اللَّـهُ الَّذِي خَلَقَ السَّمَاوَاتِ وَالْأَرْضَ فِي سِتَّةِ أَيَّامٍ ثُمَّ اسْتَوَىٰ عَلَى الْعَرْشِ ۖ يُدَبِّرُ الْأَمْرَ ۖ مَا مِن شَفِيعٍ إِلَّا مِن بَعْدِ إِذْنِهِ ۚ ذَٰلِكُمُ اللَّـهُ رَبُّكُمْ فَاعْبُدُوهُ ۚ أَفَلَا تَذَكَّرُونَ ﴿٣﴾

3. Bila shaka Mola wenu ni Mwenyezi Mungu ambaye ameziumba mbingu na ardhi katika siku sita. Kisha akatawala juu ya Arshi. Yeye ndiye anayepitisha mambo yote. Hakuna muombezi ila baada ya idhini yake. Huyu ndiye Mwenyezi Mungu, Mola wenu, basi Muabuduni yeye. Je hamkumbuki?.

Moja kati ya taratibu alizojiwekea Mwenyezi Mungu s.w.t ni kuumba ulimwengu hatua kwa hatua. Na ndiyo maana pamoja na kuwa na uwezo wa kuuumba ulimwengu na kila kiumbe wakati mmoja, Allah s.w.t aliamua kuziumba mbingu na ardhi katika nyakati sita tofauti. Na hivyo ndivyo alivyojaalia pia katika maumbile ya viumbe wengine akiwemo binaadamu ambaye pia uumbwaji wake ni wa hatua kwa hatua, toka tone la manii, pande la damu na hadi mwishowe kufikia kiumbe kamili.

Kama tunavyoona kitoto kichanga kabla ya kuja duniani hupitisha kipindi cha miezi tisa tumboni mwa mama kikiwa katika umbo na hali tofauti hadi kuwadia wakati wa kuja duniani, hali ya kuwa kama angetaka, yeye Mola aliye Muweza wa kila kitu angeufanya uumbaji wote huo katika lahadha moja tu.

Baadhi ya yale tunayojifunza katika aya hii ni kuwa uumbaji wa ulimwengu umetokana na ratiba na wakati maalumu na si jambo lililotokea kwa sadfa tu. Aidha aya inatuonyesha kuwa ulimwengu ni kitu kinachofuata kanuni na malengo maalumu. Na sababu ni kuwa mumbaji wake ni mmoja tu.

### AYA YA NNE

Darsa hii ya 306 inahitimishwa na aya ya 4 ambayo inasema:

إِلَيْهِ مَرْجِعُكُمْ جَمِيعًا ۖ وَعْدَ اللَّـهِ حَقًّا ۚ إِنَّهُ يَبْدَأُ الْخَلْقَ ثُمَّ يُعِيدُهُ لِيَجْزِيَ الَّذِينَ آمَنُوا وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ بِالْقِسْطِ ۚ وَالَّذِينَ كَفَرُوا لَهُمْ شَرَابٌ مِّنْ حَمِيمٍ وَعَذَابٌ أَلِيمٌ بِمَا كَانُوا يَكْفُرُونَ ﴿٤﴾

4. Kwake ndiyo marejeo yenu nyote. Hii ni ahadi ya Mwenyezi Mungu iliyo ya kweli. Hakika yeye ndiye aliyeanzisha viumbe na ndiye atakayewarejesha (baada ya kufa kwao) ili awalipe kwa uadilifu wale walioamini na kufanya vitendo vizuri. Na wale waliokufuru wao watapata vinywaji vya maji yanayochemka na adhabu inayoumiza kwa sababu ya kukataa kwao.

Aya iliyotangulia imeashiria uwezo wa Mwenyezi Mungu katika uumbaji wa mbingu na ardhi. Aya hii ya nne inazungumzia uumbaji wa mara ya pili wa viumbe, yaani kufufuliwa kwao siku ya kiyama; na katika kuliondolea shaka suala hilo inasema, hiyo ni ahadi ya Mwenyezi Mungu isiyo na shaka ambapo wale waliomwamini Mola wao wakatenda mema watapata jaza ya kheri, na wale waliomkufuru, malipo yao yatakuwa ni adhabu. Tabaan yote

hayo yatafanyika kwa uadilifu ambayo ni miongoni mwa sifa kuu za Allah s.w.t

Baadhi ya yale tunayojifunza kutokana na aya hii ni kuwa falsafa ya kufufuliwa viumbe ni kuthibiti kwa uadilifu wa Mwenyezi Mungu mtukufu. Kwani dunia hii ndogo na ya kupita tunayoishi haitoshi kuwa ni mahali pa kuwalipa kiadilifu wale waliomwamini Allah na kutenda mema na pia kuwapa adhabu wanayostahiki wale waliomkufuru Mwenyezi Mungu na kufanya kila aina ya dhulma. Aidha aya inatuelimisha kuwa kama dunia na kila kilichomo ndani yake kimeumbwa kwa ajili ya mwanaadamu, huko akhera pia kuwepo kwa ulimwengu huo na neema na nakama zake vitakuwepo kwa ajili ya kutoa malipo kwa sisi wanadamu kutokana na yale yaliyotangulizwa na mikono yetu. Darsa ya 306 imefikia tamati.

Tunamwomba Mwenyezi Mungu atujaalie kuwa na mwisho mwema na kutunusuru na adhabu ya moto. Amin.

## SURAT YUNUS 5-10

Bismillahir Rahmanir Rahim.

Tunamshukuru Mwenyezi Mungu mtukufu kwa kutuwafikisha kukutana tena katika darsa letu hii.

### AYA YA 5 NA 6

Sura ya 10 ya Yunus ndiyo tunayoizungumzia kwa sasa, na tunaianza kwa aya ya 5 na 6 za sura hiyo ambazo zinasema:

هُوَ الَّذِي جَعَلَ الشَّمْسَ ضِيَاءً وَالْقَمَرَ نُورًا وَقَدَّرَهُ مَنَازِلَ لِتَعْلَمُوا عَدَدَ السِّنِينَ وَالْحِسَابَ مَا
خَلَقَ اللَّـهُ ذَٰلِكَ إِلَّا بِالْحَقِّ يُفَصِّلُ الْآيَاتِ لِقَوْمٍ يَعْلَمُونَ

5. Yeye (Mwenyezi Mungu) ndiye aliyelifanya jua kuwa muanga, na mwezi kuwa nuru na akaupimia vituo(huo mwezi) ili mujue idadi ya miaka na hisabu (nyinginezo). Mwenyezi Mungu hakuviumba hivyo ila kwa haki. Anazipambanua ishara (zake) kwa watu wanaotaka kujua.

﴿٥﴾ إِنَّ فِي اخْتِلَافِ اللَّيْلِ وَالنَّهَارِ وَمَا خَلَقَ اللَّـهُ فِي السَّمَاوَاتِ وَالْأَرْضِ لَآيَاتٍ لِّقَوْمٍ يَتَّقُو نَ
﴿٦﴾

6. Hakika katika mfuatano (wa daima) wa usiku na mchana ; na katika alivyoviumba Mwenyezi Mungu katika mbingu na ardhi ziko ishara kwa watu wanaomcha Mungu.

Baada ya aya za mwanzoni mwa sura hii kuashiria juu ya kufufuliwa, kama tulivyoona katika darsa iliyopita, aya hizi tulizosoma zinagusia sehemu ndogo tu ya madhihirisho ya adhama ya Mwenyezi Mungu katika uumbaji kwa kuzungumzia nafasi ya jua na mwezi.

Uhai wa wanaadamu na sayari yenyewe ya dunia vinategemea nuru na joto litokanalo na jua kama ambavyo nuru ya kupendeza ipatikanayo kupitia kwenye mwezi huwa mithili ya mwanga wa kulalia kwa viumbe mbali mbali wakiwemo wanadamu na pia hutumiwa kama kurunzi ya kuongozea njia katika safari za majangwani na baharini za viumbe hao.

Lakini pia kama tunavyojua mwendo wa sayari ya dunia wa kulizunguka jua na ule wa mwezi wa kuizunguka dunia ndivyo vinavyotuwezesha kuwa na hesabu za siku na pia mwaka kulingana na kalenda ya jua yaani shamsia.

Aidha kutokana na mabadiliko ya umbo la mwezi kuanzia hilali hadi mwezi kamili, ndivyo tunavyoweza kupata pia hesabu ya miezi 12 kulingana na kalenda ya Hijria.

Aya zinamalizia kwa kutilia mkazo nukta hii kwamba yote hayo yaani mfumo kamili wa uumbaji vimefanywa kwa ajili ya kuthibitisha kuwa Mwenyezi Mungu ni wa haki na yote hayo ameyafanya kwa hikma kubwa na kwamba mabadiliko tunayoshuhudia kila siku ya kubadilika kwa usiku na mchana ambayo wengi wetu tunayachukulia kuwa ni kitu cha kawaida, ni dhihirisho la uwezo na hikma ya Allah s.w.t ambalo wanalidiriki na kulihisi wale wamchao yeye Mola Mwenyezi.

Baadhi ya yale tunayojifunza kutokana na aya hizi ni kuwa idadi, hesabu na tarakimu ni vitu vyenye umuhimu katika maisha ya mwanadamu, na quran inatuonyesha kuwa kuhesabu masiku ya mwezi na mwaka kwa kutumia jua na mwezi ni miongoni mwa njia za kutumia kwa ajili ya kufanyia hesabu hizo.

Funzo jengine na ambalo ni la kuzingatiwa sana katika aya hizi ni kuwa haifai kwa muislamu kuvipita vivi hivi vitu vya kimaumbile vilivyomzunguka, kwani katika vitu hivyo anaweza kushuhudia kwa karibu adhama yake Mola Muumba.

## AYA 7 NA 8

Zifuatazo sasa ni aya 7 na 8 ambazo zinasema:

إِنَّ الَّذِينَ لَا يَرْجُونَ لِقَاءَنَا وَرَضُوا بِالْحَيَاةِ الدُّنْيَا وَاطْمَأَنُّوا بِهَا وَالَّذِينَ هُمْ عَنْ آيَاتِنَا غَافِلُونَ ﴿٧﴾

7. Hakika wale wasiotaraji kukutana nasi na wakaridhia maisha ya dunia na wakatua kwa hayo, na waloghafilika na ishara zetu.

أُولَـٰئِكَ مَأْوَاهُمُ النَّارُ بِمَا كَانُوا يَكْسِبُونَ ﴿٨﴾

8. Hao makaazi yao ni motoni kwa sababu ya yale waliyokuwa wakiyachuma.

Baada ya aya zilizotangulia kubainisha ishara za kuwepo Allah s.w.t kupitia uumbaji wa mbingu na ardhi aya hizi zinasema wale walioghafilika na ishara hizo na kushindwa kuzidiriki ishara za kuwepo Mwenyezi Mungu, uwezo wake na hikma yake huishia katika kuikumbatia dunia ya kupita wakidhani kuwa kila kitu kinaishia hapa.

Hivyo huwa hawafikirii juu ya kukutana na Mola wao siku ya Kiyama, na ndiyo maana mwisho wa watu hao unakuwa ni kwenda kutumbukizwa kwenye moto wa jahannam huko akhera.

Moja kati ya mafunzo muhimu tunayoyapata kutokana na aya hizi ni kuwa kughafilika na Kiyama na kuipaparikia dunia ndiyo mambo yanayomfanya mtu atumbukie kwenye ufuska na maasi.

## AYA 9 NA 10

Darsa yetu tunaihitimisha kwa aya 9 na 10 ambazo zinasema:

إِنَّ الَّذِينَ آمَنُوا وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ يَهْدِيهِمْ رَبُّهُم بِإِيمَانِهِمْ تَجْرِي مِن تَحْتِهِمُ الْأَنْهَارُ فِي جَنَّاتِ النَّعِيمِ ﴿٩﴾

9. Hakika wale walioamini na wakatenda mema Mola wao Mlezi atawaongoa kwa sababu ya imani yao. Itakuwa inapita mito mbele yao katika mabustani yenye neema.

دَعْوَاهُمْ فِيهَا سُبْحَانَكَ اللَّـهُمَّ وَتَحِيَّتُهُمْ فِيهَا سَلَامٌ ۚ وَآخِرُ دَعْوَاهُمْ أَنِ الْحَمْدُ لِلَّـهِ رَبِّ الْعَالَمِينَ ﴿١٠﴾

10. Wito wao humo utakuwa utakuwa: Subhanakallahumma! Umetakasika Ee Mwenyezi Mungu. Na maamkiano yao humo ni salamun (Alaykum). Na wito wao wa mwisho ni: Alhamdulillahi Rabbil Aalamin" Kuhimidiwa kote ni kwa Mwenyezi Mungu. Mola Mlezi wa walimwengu wote.

Wakati aya zilizotangulia zimebainisha hali ya adhabu itakayowapata wale walioamua kuiabudu dunia, aya hizi zinaashiria hali ya waumini watakaoingizwa peponi na kusema kuwa kupata uongofu wa Allah ndiyo hazina kubwa waliyokuwa nayo watu hao tabaan waliipata kutokana na kumwamini Mola wao na kufanya amali njema.

Kisha aya zinaashiria dua na dhikri za watu wa peponi na kusema kuwa utajo wa Subhanallah na Alhamdulillah ni miongoni mwa alama za watu hao, lakini kama tujuavyo dhikri hizo haziishii katika kuzitamka kwa ulimi tu bali mtu anatakiwa awe anaitakidi kwa dhati kuwa Allah s.w.t ametakasika na kila kasoro na upungufu, na ni kwa kufahamu hivyo ndipo mja humhimidi na kumshukuru kwa dhati Mola Mwenyezi kwa sifa zake zote za ukamilifu.

Aya hizi wapenzi wasomaji zinatuoyesha kuwa uongofu wa Allah ni kitu anachokihitajia katika lahadha ya uhai wake. Aidha aya zinatuonyesha kuwa maamkizi ya amani, ndiyo yatakayotawala katika anga ya peponi. Maamkizi ya amani yatakyotoka kwa Mwenyezi Mungu, yatakayotoka kwa Malaika, na pia watakayopeana watu wa peponi wao kwa wao. Inshaallah Mwenyezi Mungu atujaalie kuwa miongoni mwa watu hao. Amin.

2

# TAFSIRI YA SUURAT YUUNUS

## SURAT YUNUS 11-14

Bismillahir Rahmanir Rahim. Tunamshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa kutuwafikisha kukutana tena katika darsa yetu hii.

### AYA YA 11

Sura ya 10 ya Yunus ndiyo tunayoizungumzia kwa sasa, na hapa tunaianza kwa aya ya 11 ambayo inasema:

وَلَوْ يُعَجِّلُ اللَّـهُ لِلنَّاسِ الشَّرَّ اسْتِعْجَالَهُم بِالْخَيْرِ لَقُضِيَ إِلَيْهِمْ أَجَلُهُمْ فَنَذَرُ الَّذِينَ لَا يَرْجُونَ لِقَاءَنَا فِي طُغْيَانِهِمْ يَعْمَهُونَ ﴿١١﴾

11. Na lau kama Mwenyezi Mungu angeliwafanyia watu haraka kuwaletea shari, kama wanavyojihimizia kuletewa kheri, bila shaka wangelisha timiziwa ajali yao. Lakini tunawaacha wale wasiotumainia kukutana nasi, wakihangaika katika upotovu wao.

Moja ya utaratibu ambao Allah s.w.t ameuweka kuhusiana na waja wake ni kutoa muhula na fursa kwao, ili kila mmoja aamue na kuchagua kwa hiyari yake njia gani anayotaka kufuata, ikiwa ni ya kuiamini haki au kuikufuru. Kwa bahati mbaya akthari ya watu huwa hawaitumii kwa njia sahihi fursa hiyo adhimu wanayotunukiwa na Mola wao, na badala yake huogelea kwenye dimbwi la maasi na maovu. Pamoja na hayo Mola aliye mrehemevu huendelea kuamiliana kwa upole na ukarimu na waja wake kwa kuwapa fursa nyingine ya kutubia kwa madhambi waliyoyafanya ili wapate maghufira na msamaha wake.

Ama ikiwa hata baada ya kupata fursa hiyo mja ataamua kuselelea katika kutenda maovu na kumwasi Mola Muumba, mja wa aina hiyo huachwa kama alivyo aendelee kufuata njia hiyo ya upotofu hadi kipindi cha uhai wake kinapomalizika, ambapo hapo huelekea ulimwengu mwingine wa akhera na huko hupata jaza na malipo ya maovu na maasi aliyoyafanya hapa duniani.

Aya hii pamoja na mambo mengine inatufunza kuwa kutoangamizwa kwa makafiri na madhalimu hapa duniani hakumaanishi kuwa yale wayafanyao ni ya sawa au kwamba Mwenyezi Mungu sw anashindwa kuwateremshia adhabu. Bali hiyo inatokana na ile fursa na muhula ambao Allah ameamua kuwapa waja wake hao.

### AYA YA 12

Ifuatayo sasa ni aya ya 12 ambayo inasema:

وَإِذَا مَسَّ الْإِنسَانَ الضُّرُّ دَعَانَا لِجَنبِهِ أَوْ قَاعِدًا أَوْ قَائِمًا فَلَمَّا كَشَفْنَا عَنْهُ ضُرَّهُ مَرَّ كَأَن لَّمْ يَدْعُنَا إِلَىٰ ضُرٍّ مَّسَّهُ ۚ كَذَٰلِكَ زُيِّنَ لِلْمُسْرِفِينَ مَا كَانُوا يَعْمَلُونَ ﴿١٢﴾

12. Na mtu akiguswa na shida hutuomba, naye kaegesha ubavu, au kakaa, au kasimama. Lakini tukimwondoshea shida yake huendelea kama kwamba hakupata kutuomba tumwondoshee shida iliyompata. Namna hivi wamepambiwa warukao mipaka yale waliyokuwa wakiyatenda.

Raha na neema za kidunia wapenzi wasomaji humfanya mtu aghafilike na Mola wake na kuikumbatia dunia. Ama shida, masaibu na matatizo mara

nyingi humfumbua macho mtu huyo na kumfanya aelewe kuwa binadamu ni kiumbe dhaifu kiasi kwamba pale anapotingwa na matatizo hutambua jinsi ya kumwomba na kumlingana Mwenyezi Mungu kutaka msaada, awe kitandani anaugua maradhi akiomba aponywe, au baharini na angani pale mauti yanapomkabili akawa hana njia nyingine yoyote ya kujiokoa, na hivyo kutaka nusra ya Mwenyezi Mungu s.w.t

Ya laiti baada ya mja kuitikiwa kilio chake hicho angeweza walau kumshukuru tu Mola wake na kuendelea kumkumbuka japo kwa siku chache.

Lakini wapi! Akthari ya watu humsahau haraka Mwenyezi Mungu kana kwamba hawakuwa wametingwa na masaibu na ni yeye Mola aliyetukuka ndiye aliyewaondolea masaibu hayo.

Baadhi ya mafunzo tunayoyapata kutokana na aya hii ni kuwa imani ya kuwepo na Mungu mmoja imekita ndani ya nafsi ya kila mwanadamu, na kwa kweli maafa, shida na misukosuko huwa ndiyo chachu ya kuiamsha fitra na maumbile hayo yaliyolala ya kukiri kuweo kwa yule aliye na uwezo mutlaki wa kila kitu.

### AYA YA 13 NA 14

Aya ya 13 na 14 ndizo zinazotuhitimishia darsa letu hii. Aya hizo zinasema:

وَلَقَدْ أَهْلَكْنَا الْقُرُونَ مِن قَبْلِكُمْ لَمَّا ظَلَمُوا ۙ وَجَاءَتْهُمْ رُسُلُهُم بِالْبَيِّنَاتِ وَمَا كَانُوا لِيُؤْمِنُوا ۚ كَذَٰلِكَ نَجْزِي الْقَوْمَ الْمُجْرِمِينَ ﴿١٣﴾

13. Na kwa yakini tumekwisha ziangamiza uma nyingi kabla yenu walipodhulumu, na waliwajia Mitume wao kwa hoja zilizowazi; lakini hawakuwa wenye kuamini. Namna hivi tunawalipa watu wanaofanya waovu.

ثُمَّ جَعَلْنَاكُمْ خَلَائِفَ فِي الْأَرْضِ مِن بَعْدِهِمْ لِنَنظُرَ كَيْفَ تَعْمَلُونَ ﴿١٤﴾

14. Kisha tukakufanyeni nyinyi ndio wenye kushika mahala pao baada yao katika ardhi ili tuone jinsi mtakavyotenda.

Ijapokuwa kama tulivyotangulia kunena katika aya zilizotangulia Mwenyezi Mungu huwapa muhula wale wanaomwasi na kufanya madhambi na kutowaangamiza papa hapa duniani, lakini hili huwa ni tofauti linapohusu umma au kaumu nzima ya watu, pale watu hao wanapokithirisha dhulma na madhambi, kwani hatima ya kaumu za aina hiyo ni kuangamizwa. Kisha baada ya kuangamizwa kaumu hizo huletwa mahala pao kaumu ya watu wengine ambao wanatakiwa kuyachukulia yale yaliyowasibu waliowatangulia kuwa ni ibra na funzo kwao, vinginevyo na wao pia watapatwa na majaaliwa kama yao.

Miongoni mwa mafunzo tunayoyapata kutokana na aya hizi ni kuwa dhulma na uonevu ni mambo yanayoandaa mazingira ya kuangamizwa watu, tabaan wale watu ambao hakuna matumaini tena kwa wao kuamini na kuifuata haki.

Halikadhalika aya zinatuelimisha kuwa hatima na majaaliwa ya watu yako mikononi mwao wenyewe, na kwa kweli ni matendo yao mabaya na maovu ndiyo yanayoainisha wawe na hatima gani.

Na pia aya zinatufunza kwamba endapo mtu atajiona amepata madaraka au mamlaka ya utawala, ajue kuwa huo ni mtihani ambao Mwenyezi Mungu amempa kumjaribu. Tunamwomba Allah atuwafikishe kufuzu mitihani yake na atuzindue kila pale tunapoghafilika na kumkumbuka yeye. Amin.

## SURAT YUNUS 15-18

Tunamshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa kutuwafikisha kukutana tena katika darsa letu hii.

### AYA YA 15

Sura ya 10 ya Yunus ndiyo tunayoizungumzia kwa sasa, na hili ni darsa la 309, tunayoianza kwa aya ya 15 ambayo inasema:

وَإِذَا تُتْلَىٰ عَلَيْهِمْ آيَاتُنَا بَيِّنَاتٍ ۙ قَالَ الَّذِينَ لَا يَرْجُونَ لِقَاءَنَا ائْتِ بِقُرْآنٍ غَيْرِ هَـٰذَا أَوْ بَدِّلْهُ ۚ قُلْ مَا يَكُونُ لِي أَنْ أُبَدِّلَهُ مِن تِلْقَاءِ نَفْسِي ۖ إِنْ أَتَّبِعُ إِلَّا مَا يُوحَىٰ إِلَيَّ ۖ إِنِّي أَخَافُ إِنْ عَصَيْتُ رَبِّي عَذَابَ يَوْمٍ عَظِيمٍ ﴿١٥﴾

15. Na wanaposomewa aya zetu zilizo wazi, wale wasiotaraji kukutana nasi husema: Lete quran isiyokuwa hii au ibadilishe. Sema: Siwezi kuibadilisha kwa hiyari ya nafsi yangu. Mimi sifuati ila ninayofunuliwa kwa Wahyi. Hakika mimi naogopa nikumuasi Mola wangu adhabu ya siku iliyo kuu.

Washirikina na waabudu masanamu ambao walikuwa walinganiwa wa wito wa tauhidi aliokuja nao Bwana Mtume Muhammad **(s.a.w.w)**, badala ya kuachana na itikadi na ibada zao hizo potofu, ni wao ndio waliomtaka bwana Mtume akidhi matakwa yao kwa kuzifuta katika Quran zile aya zinazokataza na kukemea ibada ya masanamu, au hata ikiwezekana kuleta kitabu kingine kabisa kisicho na aya za aina hiyo, ili hapo ndipo wao wamwamini Mtume huyo wa Allah.

Hali ya kuwa lengo la Mitume ni kuwaelekeza watu kwenye uongofu na si kutaka kujipatia wafuasi wengi zaidi. Kwa maana kwamba katu hawawezi kukubali matakwa yasiyo ya kimantiki ya watu kwa sababu tu ya kutaka kupata idadi kubwa zaidi ya wafuasi.

Baadhi ya mafunzo tunayoyapata kutokana na aya hii ni kuwa hakuna mtu yeyote yule hata Mtume aliye na haki ya kuibadilisha hata aya moja ya vitabu vya mbinguni vilivyoteremshwa na Allah, bali manabii hao, wao wenyewe ni wenye kujisalimisha na kutii kikamilifu kila kilichokuja katika risala ya wahyi walioteremshiwa na Mola wao.

Aidha aya inatuelimisha kuwa msingi wa mafundisho ya Uislamu ni kushikamana nayo kama yalivyo yale yaliyoletwa na Mwenyezi Mungu, na wala hakuna thamani yoyote kuifanya dini iwe na wafuasi wengi zaidi kwa gharama ya kubadilisha na kupotosha mafundisho yake ya asili.

### AYA ZA 16 NA 17

Zifuatazo sasa ni aya za 16 na 17 ambazo zinasema:

قُل لَّوْ شَاءَ اللَّـهُ مَا تَلَوْتُهُ عَلَيْكُمْ وَلَا أَدْرَاكُم بِهِ ۖ فَقَدْ لَبِثْتُ فِيكُمْ عُمُرًا مِّن قَبْلِهِ ۚ أَفَلَا تَعْقِلُونَ ﴿١٦﴾

16. Sema: Mwenyezi Mungu angeli taka nisingeli kusomeeni, wala nisingeli kujuvyeni. Kwani nilikwisha kaa nanyi umri mzima kabla yake! Basi, je hamzingatii?

فَمَنْ أَظْلَمُ مِمَّنِ افْتَرَىٰ عَلَى اللَّـهِ كَذِبًا أَوْ كَذَّبَ بِآيَاتِهِ ۚ إِنَّهُ لَا يُفْلِحُ الْمُجْرِمُونَ ﴿١٧﴾

17. Basi ni nani dhalimu zaidi kuliko yule anayemzulia uwongo Mwenyezi Mungu na akazikanusha aya zake? Hakika hawafaulu wale wafanyao maovu.

Aya hizi wapenzi wasomaji zinaendelea kutoa jibu kwa wale watu waliomtaka Bwana Mtume Muhammad **(s.a.w.w)** aibadilishe quran na kuwaambia, Mtume huyu ameishi na nyinyi kwa miaka arubaini.

Lau quran hii ingekuwa imetokana na fikra zake yeye mwenyewe bila shaka katika kipindi hicho chote mungeweza kushuhudia maneno mithili ya hayo katika fikra zake. Isitoshe ni kuwa yeye Muhammad hakuwahi kusoma popote wala kufunzwa na yeyote hata mseme labda hii quran itakuwa ni matunda ya elimu hiyo aliyokuwa amejifunza hapo kabla.

Hivyo wale wanomtaka yeye aibadilishe quran hakika wanachofanya ni kuzikadhibisha aya za Mwenyezi Mungu na kumzulia uwongo yeye Mola Muumba, jambo ambalo ni sawa na kumfanyia dhulma kubwa kabisa yeye Mola, Mtume wake na kitabu chake cha quran.

Baadhi ya tunayojifunza katika ya hizi ni kuwa vitabu vya mbinguni ni wahyi utokao moja kwa moja kwa Allah na wala si kitu kinachotokana na fikra za Mitume au mtu mwengine yoyote.

Aidha zinatutaka tuelewe kuwa dhulma kubwa kabisa ni ile ya kupotosha na kuyabadilisha mafundisho asili ya dini.

## AYA YA 18

Tunaihitimisha darsa yetu hii kwa aya ya 18 ambayo inasema:

وَيَعْبُدُونَ مِن دُونِ اللَّـهِ مَا لَا يَضُرُّهُمْ وَلَا يَنفَعُهُمْ وَيَقُولُونَ هَـٰؤُلَاءِ شُفَعَاؤُنَا عِندَ اللَّـهِ ۚ قُلْ أَتُنَبِّئُونَ اللَّـهَ بِمَا لَا يَعْلَمُ فِي السَّمَاوَاتِ وَلَا فِي الْأَرْضِ ۚ سُبْحَانَهُ وَتَعَالَىٰ عَمَّا يُشْرِكُونَ ﴿١٨﴾

18. Nao wanaabudu (waungu) wasiokuwa Mwenyezi Mungu wasioweza kuwadhuru wala kuwanufaisha. Na wanasema: "Hao ndio waombezi wetu kwa Mwenyezi Mungu". Sema:"Je Mnamwambia Mwenyezi Mungu asiyoyajua katika mbingu wala katika ardhi?".Ameepukana na upungufu (wa kutaka mshirika), na ametukuka na hao wanaowashirikisha naye.

Washirikina walikuwa wakiyaabudu masanamu ambayo si kwamba yalikuwa yana uwezo wa kuwadhuru hata kwa kukhofia hilo wahisi kuwa hawana budi ila kuwaabudu, na si kwamba pia kuna faida walikuwa wakipata kwa masanamu hayo hata tamaa ya kupata faida hiyo iwe sababu ya kuwafanya wawapigie magoti na kuwaomba.

Ama hoja waliyokuwa wakiitoa washirikina hao ni kuwa masanamu hayo yalikuwa ni wasita na kiunganishi kati yao na Mwenyezi Mungu.

Hata hivyo hoja hii haikubaliki kwa sababu Mwenyezi Mungu hakuyafanya masanamu hayo ni wasita, kiunganishi na waombezi wa waja wake kwake yeye. Hii ni tofauti na wala haiwezi kulinganishwa na suala la tawasul wanayofanya watu kwa Mitume na mawalii wa Mwenyezi Mungu na kuomba wawatakie shufaa mbele ya Mola, kwani hao wako katika maisha maalumu ya barzakhi waliyojaaliwa na Allah na vile vile ni yeye

Mola mwenyewe aliyewaelekeza watu watumie wasita wa waja wake hao walio wateule kwa ajili ya kumfikia yeye.

Funzo moja muhimu tunalolipata kutokana na aya hii ni kuwa tujihadhari na kukifanya kitu au mtu yeyote yule kuwa mshirika wa Allah katika uungu, au kukifanya kitu au mtu kuwa na hadhi ya kuweza kutushufaia na kutuombea mbele ya yeye Mola, ghairi ya wale yeye Allah mwenyewe aliowapa daraja hiyo ya kuwa waombezi kwa waja wake.

Darsa ya 309 imefikia tamati. Tunamwomba Allah atulinde na kila aina ya shirki. Amin.

3

# TAFSIRI YA SUURAT YUUNUS

## SURAT YUNUS 19-23

Bismillahir Rahmanir Rahim. Assalaamu Warahmatullahi Wabarakaatuh. Karibuni katika mfululizo mwingine wa Darsa ya Qur'an.

### AYA YA 19

Hii ni darsa ya 310, na tukiwa tunaendelea kuizungumzia sura ya 10 ya Yunus, tunaianza darsa yetu kwa aya ya 19 ambayo inasema:

وَمَا كَانَ النَّاسُ إِلَّا أُمَّةً وَاحِدَةً فَاخْتَلَفُوا ۚ وَلَوْلَا كَلِمَةٌ سَبَقَتْ مِن رَّبِّكَ لَقُضِيَ بَيْنَهُمْ فِيمَا فِيهِ يَخْتَلِفُونَ ﴿١٩﴾

19. Wala watu hawakuwa ila umma mmoja tu. Kisha wakakhitalifiana. Na lau kuwa si neno lililo kwisha tangulia kutoka kwa Mola wako, bila shaka hukumu ingelikwisha katwa baina yao katika hayo wanayo khitalifiana.

Mwenyezi Mungu sw amewaumba wanaadamu wote wakiwa na fitra yaani maumbile safi ya tauhidi ya kukubali kuwepo kwa Mungu mmoja.

Hivyo hapo awali wanaadamu wote walikuwa ni sawa na umma mmoja. Lakini kwa kupita muda, na kuzainiwa na shetani kundi miongoni mwa watu wakatumbukia kwenye upotofu wa shirki na hivyo watu wakagawika katika makundi mawili ya wampwekeshao Allah na Mushrikina. Ama Mwenyezi Mungu hakutaka kuwateza nguvu waja wake, bali alitaka kila mtu achague kwa hiyari yake njia anayoamua kufuata. Na ni kwa sababu hiyo ndipo akaamua kuwapa fursa na muhula wale waliokhitari upotofu kufanya lolote lile watakalo.

Na lau si utaratibu huo aliouweka Mwenyezi Mungu basi angewaadhibu papa hapa duniani na kumaliza hitilafu kati ya waumini na makafiri. Funzo mojawapo tunalopata katika aya hii ni kuwa thamani na utukufu wa mwanadamu unapatikana kwa kule kufanya ayatakayo ikiwa ya thawabu au ya madhambi kwa hiyari yake. Vinginevyo hakuna fakhari yoyote kwa mtu kuamini na kufuata njia ya haki kwa kulazimishwa.

### AYA YA 20

Ifuatayo sasa ni aya ya 20 ambayo inasema:

وَيَقُولُونَ لَوْلَا أُنزِلَ عَلَيْهِ آيَةٌ مِّن رَّبِّهِ ۖ فَقُلْ إِنَّمَا الْغَيْبُ لِلَّهِ فَانتَظِرُوا إِنِّي مَعَكُم مِّنَ الْمُنتَظِرِينَ ﴿٢٠﴾

20. Na wanasema: Kwa nini hakuteremshiwa kutoka kwa Mola wake miujiza (tunayoitaka)? Sema: Mambo ya ghaibu ni ya Mwenyezi Mungu.Basi nyinyi ngojeni, na mimi ni pamoja na nanyi katika wanaongoja.

Nabii Muhammad **(s.a.w.w)** alikuja na miujiza mbali mbali kama walivyokuwa Manabii waliomtangulia. Tabaan muujiza mkuu wa Mtume huyo wa mwisho ni quran tukufu ambao washirikina walishindwa kukabiliana nao hata kwa kuleta walau aya moja mfano wake.

Lakini katika kutafuta visingizio, washirikina hao kila siku walikuwa wakitaka waonyeshwe muujiza mpya ikiwa ni pamoja na kumtaka Bwana Mtume awaletee kila wanachotaka. Ndipo katika kuwajibu Bwana Mtume

akawaambia muujiza ni suala lililoko kwenye mamlaka ya Mwenyezi Mungu na wala haliko mikononi mwangu mimi, na ni kila pale anapotaka yeye ndipo muujiza unapoletwa, ama mnachotaka nyinyi si kitu kingine ghairi ya kutafuta visingizio tu.

Ukweli wa haya wapenzi wasomaji unashuhudiwa pia kama tulivyoona katika aya zilizotangulia pale washirikina wa kikureishi walipomtaka Bwana Mtume azibadilishe aya za quran au hata ikiwezekana awaletee qurani nyingine mpya badala ya ile aliyoteremshiwa na Mola wake.

Pamoja na mambo mengine aya hii inatufunza kuwa chanzo na chimbuko la shirki na ukafiri si kutokuwepo muujiza na hoja za kuthibitisha ukweli wa risala ya haki, isipokuwa ni tabia ya ukaidi, inda na inadi mbele ya haki.

### AYA YA 21

Tunaiendeleza darsa yetu kwa aya ya 21 ambayo inasema:

وَإِذَا أَذَقْنَا النَّاسَ رَحْمَةً مِّن بَعْدِ ضَرَّاءَ مَسَّتْهُمْ إِذَا لَهُم مَّكْرٌ فِي آيَاتِنَا ۚ قُلِ اللَّهُ أَسْرَعُ مَكْرًا ۚ إِنَّ
رُسُلَنَا يَكْتُبُونَ مَا تَمْكُرُونَ ﴿٢١﴾

21. Na tunapowaonjesha watu rehma baada ya shida iliyowapata, mara huanza kutunga hila (za kutaka kupinga) Aya zetu. Sema: Mwenyezi Mungu ni mwepesi zaidi wa kupanga. Hakika wajumbe wetu wanayaandika mnayoyapanga.

Historia inasimulia kuwa ilitokea wakati mmoja mji wa Makka ulikumbwa na ukame mkubwa lakini Mwenyezi Mungu kwa baraka ya kuwepo Nabii Muhammad **(s.a.w.w)** akateremsha mvua zake za rehma na kuuletea faraja mji huo.

Ama washirikina wao walidai kuwa kunyesha kwa mvua hizo kulitokana na baraka za masanamu yao.

Ndipo aya tuliyoisoma ikashuka na kuwatanabahisha kuwa kama nyinyi ni wenye kutaka hakika ya mambo, basi tambueni kuwa mvua hizo ilikuwa ni muujiza utokao kwa Mwenyezi Mungu. Hata hivyo inadi yenu imekufanyeni muzue hila hizi na zile za kuzinasibisha na masanamu yenu rehma hiyo iliyotoka kwa Mola wenu.

Pamoja na hayo tambueni kuwa malaika wa Mwenyezi Mungu ambao hutumwa kwa watu wanayanakili na kuyarekodi yote yanayotendwa na waja na hivyo mushirikina wajiandae na majibu ya kwenda kumpa Mola wao siku ya kiyama kwa yote wanayoyatenda.

Tabaan katika dunia hii pia Mwenyezi Mungu atawapa jaza ya vitimbi na hila zao, nao katu hawawezi kusimama dhidi ya irada ya Allah s.w.t.

### AYA ZA 22 NA 23

Aya za 22 na 23 ndizo zinazotuhitimishia darsa yetu hii. Aya hizo zinasema:

هُوَ الَّذِي يُسَيِّرُكُمْ فِي الْبَرِّ وَالْبَحْرِ ۖ حَتَّىٰ إِذَا كُنتُمْ فِي الْفُلْكِ وَجَرَيْنَ بِهِم بِرِيحٍ طَيِّبَةٍ وَفَرِحُوا بِهَا
جَاءَتْهَا رِيحٌ عَاصِفٌ وَجَاءَهُمُ الْمَوْجُ مِن كُلِّ مَكَانٍ وَظَنُّوا أَنَّهُمْ أُحِيطَ بِهِمْ ۙ دَعَوُا اللَّهَ مُخْلِصِينَ لَهُ
الدِّينَ لَئِنْ أَنجَيْتَنَا مِنْ هَٰذِهِ لَنَكُونَنَّ مِنَ الشَّاكِرِينَ ﴿٢٢﴾

22. Yeye ndiye anayekuendsheni bara na baharini. Hata mnapokuwa majahazini na yakawa yanakwenda nao kwa upepo mzuri wakaufurahia,

mara upepo mkali ukawazukia na yakawajia mawimbi kutoka kila upande na wakaona wameshatingwa, hapo ndipo wanapomwomba Mwenyezi Mungu kwa kumtakasia utii (wakisema): Ukituokoa na haya bila shaka tutakuwa miongoni mwa wanaoshukuru.

فَلَمَّا أَنجَاهُمْ إِذَا هُمْ يَبْغُونَ فِي الْأَرْضِ بِغَيْرِ الْحَقِّ يَا أَيُّهَا النَّاسُ إِنَّمَا بَغْيُكُمْ عَلَىٰ أَنفُسِكُم
مَّتَاعَ الْحَيَاةِ الدُّنْيَا ثُمَّ إِلَيْنَا مَرْجِعُكُمْ فَنُنَبِّئُكُم بِمَا كُنتُمْ تَعْمَلُونَ ﴿٢٣﴾

23. Lakini akishawaokoa mara wanafanya jeuri tena katika ardhi bila ya haki.Enyi watu! Jeuri zenu zitakudhuruni wenyewe. Ni starehe (chache tu) za maisha ya dunia. Kisha marejeo yenu ni kwetu, na hapo tutakuambieni mliyokuwa mkiyatenda.

Bila shaka mngali mnakumbuka wapenzi wasomaji kuwa tulisema mwanzoni mwa darsa yetu hii kuwa Mwenyezi Mungu amewaumba wanaadamu wote katika fitra na maumbile safi ya tauhidi ya laa ilaha illa llah, yaani kukana waungu wengine wote bandia na kuthibitisha hakika ya kuwepo kwa Mola mmoja tu wa haki.

Baada ya kueleza hayo, aya hizi tulizosoma hivi punde zinabainisha kuwa mapumbao haya na yale ya kidunia huwa mithili ya utando unaogubika na kufifiliza nuru hiyo ya tauhidi ndani ya nafsi ya mtu na kumfanya mja aghafilike na Mola wake.

Ama pale mtu anapotingwa na kupatwa masaibu yanayomfanya akate tamaa ya kupata nusra kupitia njia yoyote ile hapo ndipo utando ule unapotoweka mithili ya vumbi lililosukumwa na upepo na kuiamsha fitra na maumbile ya tauhidi, na kumshuhudia mja akimlingana na kumwomba kwa ikhlasi na unyenyekevu Mola wake aliyemuumba msaada wa nusra na uokozi.

Lakini kama tulivyowahi kuashiria katika moja ya darsa zilizopita baada ya kupata nusra ya Allah mwanadamu husahau kila kitu mara moja, akighafilika kwamba maisha haya ya dunia ni mafupi na ya kupita tu, na kwamba sisi sote mwisho wetu na marejeo yetu ni kwa Mwenyezi Mungu, na huko kila mmoja atasimamishwa mbele ya mahakama ya uadilifu ili kuwajibika kwa yote aliyoyafanya hapa duniani.

Aya hizi zinatuoenyesha kuwa majanga ya kimaumbile husaidia kuondoa ghururi na kiburi cha mwanadamu na kuamsha hisia za kumtambua na kumnyenyekea Mola wake.

Aidha aya zinatutaka tuelewe kuwa imani ya msimu na ya mazingira fulani haina faida; imani ya kweli ni ya kudumu na ya katika kila hali, awe mtu katika raha na neema au shida na nakama.

Darsa ya 310 inaishia hapa. Tunamwomba Mwenyezi Mungu atujaalie kuwa miongoni mwa wale wanaomwamini na kuikiri tauhidi katika hali zote. Amin. Wassalaamu Alaykum Warahmatullahi Wabarakaatuh.

## SURAT YUNUS 24-27

Tunamshukuru Mwenyezi Mungu mtukufu kwa kutuwafikisha kukutana tena katika darsa yetu hii.

### AYA YA 24

Sura ya 10 ya Yunus ndiyo tunayoizungumzia kwa sasa, na hii ni darsa ya 311 tunayoianza kwa aya ya 24 ambayo inasema:

إِنَّمَا مَثَلُ الْحَيَاةِ الدُّنْيَا كَمَاءٍ أَنزَلْنَاهُ مِنَ السَّمَاءِ فَاخْتَلَطَ بِهِ نَبَاتُ الْأَرْضِ مِمَّا يَأْكُلُ النَّاسُ
وَالْأَنْعَامُ حَتَّىٰ إِذَا أَخَذَتِ الْأَرْضُ زُخْرُفَهَا وَازَّيَّنَتْ وَظَنَّ أَهْلُهَا أَنَّهُمْ قَادِرُونَ عَلَيْهَا أَتَاهَا أَمْرُنَا لَيْلًا
أَوْ نَهَارًا فَجَعَلْنَاهَا حَصِيدًا كَأَن لَّمْ تَغْنَ بِالْأَمْسِ كَذَٰلِكَ نُفَصِّلُ الْآيَاتِ لِقَوْمٍ يَتَفَكَّرُونَ ﴿٢٤﴾

24. Hakika mfano wa maisha ya dunia ni kama maji tuliyoyateremsha kutoka mawinguni, kisha mimea ya ardhi wanayoila watu na wanyama ikachanganyika nayo (maji hayo, ikastawi). Hata ardhi ilipokamilika uzuri wake na ikapambika, na wenyewe wakadhani wameshaiweza, iliifikia amri yetu usiku au mchana na tukaifanya kama iliyofyekwa, kama kwamba haikuwako jana. Namna hivi tunazipambanua aya (zetu) kwa watu wanaofikiri.

Katika kubainisha baadhi ya masuala, Mwenyezi Mungu ametumia ndani ya quran lugha ya tamthili na tashbihi. Aya tuliyoisoma ni miongoni mwa aya hizo ambayo imelinganisha na kushabihisha hali ya kupita na kumalizika haraka dunia kuwa ni sawa na ardhi iliyonawiri kutokana na kunyeshewa na mvua lakini pale inapokuja kukumbwa na kimbunga au mafuriko tahamaki kila kitu kilichopandwa katika ardhi hiyo kinatoweka kana kwamba havukiwepo hapo kabla.

Aya hii wapenzi wasomaji inatuelimisha kuwa umri wa mwanadamu katika dunia hii ni mfupi mithili ya umri wa mimea na maua hivyo tusihadaike tukadhani kuwa tutabaki milele katika ulimwengu huu.

### AYA YA 25

Ifuatayo sasa ni aya ya 25 ambayo inasema:

وَاللَّهُ يَدْعُو إِلَىٰ دَارِ السَّلَامِ وَيَهْدِي مَن يَشَاءُ إِلَىٰ صِرَاطٍ مُّسْتَقِيمٍ ﴿٢٥﴾

25. Na Mwenyezi Mungu anaita kwendea nyumba ya amani, na humuongoa amtakaye kwenye njia iliyonyooka (maadamu anakubali uwongofu).

Mkabala wa maisha haya ya mafupi na ya kupita ya dunia kuna maisha mengine ya milele ya akhera ambayo Mwenyezi Mungu amewataka waja wake wayapiganie hayo na akawapelekea Mitume pia wa kuongoza watu kuelekea kwenye makazi ya utulivu wa kweli.

Ni wazi kuwa watu wanaoshikamana na kamba ya uongofu ni wale ambao Mwenyezi Mungu amewahisi kuwa wana ustahili wa kufikia makazi hayo na ambao matendo na amali zao hapa duniani hazikuwa sababu ya kujiweka mbali na njia iliyonyooka.

Aya hii inatufunza kuwa raha na uzima wa dunia ni vitu vya kupita tu, kinyume chake raha na uzima wa akhera ni za kudumu na za milele. Funzo jengine tunalolipata katika aya hi ni kuwa njia pekee ya kufikia kwenye utulivu na raha za kweli ni kupiga hatua kuelekea kwenye njia ya iliyonyooka ya Allah, ambayo hapa duniani huupa moyo wa mja utulivu na huko akhera humuongoza kuelekea kwenye pepo ya saada.

### AYA YA 26

Tuitegee sikio sasa aya ya 26 ambayo inasema:

لِّلَّذِينَ أَحْسَنُوا الْحُسْنَىٰ وَزِيَادَةٌ ۖ وَلَا يَرْهَقُ وُجُوهَهُمْ قَتَرٌ وَلَا ذِلَّةٌ ۚ أُولَٰئِكَ أَصْحَابُ الْجَنَّةِ ۖ هُمْ
فِيهَا خَالِدُونَ ﴿٢٦﴾

26. Wale waliofanya wema watapata (jaza ya) wema (wao) na ziada; Wala vumbi halitawafunika nyuso zao wala madhila. Hao ndio watu wa Peponi; humo watakaa milele.

Baada ya aya iliyotangulia kuashiria juu ya pepo, aya hii inasema Mwenyezi Mungu ameiandaa pepo hiyo kwa wale waja wake waliofanya mema, na kwamba jaza na malipo watakayopata waja hao iwe ni kwa sura ya wingi au ubora, yatakuwa makubwa na bora zaidi kuliko amali walizotenda hapa duniani, .kama ambavyo katika aya nyinginezo Allah s.w.t anasema yeyote atendaye jema moja hupata thawabu na malipo mara kumi ya jema hilo, ambapo kwa upande wa utoaji, malipo ya mja hufikia hata mara mia saba ya kile alichotoa.

Baadhi ya yale tunayojifunza katika aya hii ni kuwa ikiwa Mwenyezi Mungu ametuita tuifuate njia yake ya uongofu kisha akatuonyesha njia ya kuifikia, na kisha akatushajiisha na hata kuwalipa thawabu na malipo bora kabisa wale wanaoifikia njia hiyo, ni kitu gani basi cha kutufanya tuache kuitikia mwito wa Mola wetu na kuwafuata wengine wasiokuwa yeye?

### AYA YA 27

Aya inayotuhitimishia darsa yetu ni aya ya 27 na ambayo inasema:

وَالَّذِينَ كَسَبُوا السَّيِّئَاتِ جَزَاءُ سَيِّئَةٍ بِمِثْلِهَا وَتَرْهَقُهُمْ ذِلَّةٌ ۖ مَّا لَهُم مِّنَ اللَّـهِ مِنْ عَاصِمٍ ۖ كَأَنَّمَا
أُغْشِيَتْ وُجُوهُهُمْ قِطَعًا مِّنَ اللَّيْلِ مُظْلِمًا ۚ أُولَـٰئِكَ أَصْحَابُ النَّارِ ۖ هُمْ فِيهَا خَالِدُونَ ﴿٢٧﴾

27. Na wale waliochuma maovu, malipo ya uovu ni mfano wake vile vile; na yatawafika madhila. Hawatakuwa na awezaye kuwalinda na (adhabu ya) Mwenyezi Mungu. Zitakuwa nyuso zao kama kwamba zimefunikwa na vipande vya usiku wa giza. Hao ndio watu wa Motoni; humo watakaa daima.

Wakati ambapo wale waliotenda matendo mazuri watakuwa na mwisho mwema huko akhera, wale waliokhitari kufuata upotofu kwa kumkufuru na kumwasi Mola wao hawatapata jaza nyingine ghairi ya adhabu ya Allah, na wala hawatoweza, wala kupata pa kukimbilia, ambapo ukali wa adhabu watakayopata utazifanya nyuso zao zititie na kupiga weusi.

Tabaan adhabu hiyo italingana kabisa na uzito na kiwango cha madhambi waliyofanya, ama kwa upande wa watenda mema wao watapata fadhila zake Mola za kulipwa malipo ya kheri yaliyo makubwa zaidi ya mema waliyotenda.

Aya hii pamoja na mambo mengine inatuelimisha kuwa Mwenyezi Mungu amewaumba wanaadamu akiwa amewapa uhuru na hiyari ya kuchagua njia ya kufuata. Na ndiyo maana kundi moja linaamua kufuata mema na jengine linakhitari kufuata maovu.

Halikadhalika aya inatufunza kuwa katika mfumo wa malezi wa Uislamu siku zote ushajiishaji kwa kutoa hidaya na zawadi unapewa kipaumbele kuliko utiaji adabu na utoaji adhabu.

Darsa ya 311 inaishia hapa. Tunamwomba Allah ajaalie bora ya amali zetu ziwe ni zile za lahadha ya mwisho ya uhai wetu, na siku bora kwetu iwe ni ile ya kukutana na yeye. Amin

Wassalaamu Alaykum Warahmatullahi Wabarakaatuh.

## SURAT YUNUS 28-33

Assalaamu Warahmatullahi Wabarakaatuh. Karibuni katika mfululizo mwingine wa Darsa ya Qur'an.

### AYA ZA 28 NA 29

Hii ni darsa ya 312, na tukiwa tunaendelea kuizungumzia sura ya 10 ya Yunus, tunaianza darsa yetu kwa aya za 28 na 29 ambazo zinasema:

وَيَوْمَ نَحْشُرُهُمْ جَمِيعًا ثُمَّ نَقُولُ لِلَّذِينَ أَشْرَكُوا مَكَانَكُمْ أَنتُمْ وَشُرَكَاؤُكُمْ ۚ فَزَيَّلْنَا بَيْنَهُمْ ۖ وَقَالَ شُرَكَاؤُهُم مَّا كُنتُمْ إِيَّانَا تَعْبُدُونَ ﴿٢٨﴾

28. Na siku tutakapowakusanya wote, kisha tutawaambia wale walioshirikisha: 'Simameni mahali penu nyinyi na wale mliowafanya washirika wa Mungu.' Kisha tutawatenga baina yao. Na hao waliowashirikisha watasema: 'Nyinyi hamkuwa mkituabudu sisi.

فَكَفَىٰ بِاللَّهِ شَهِيدًا بَيْنَنَا وَبَيْنَكُمْ إِن كُنَّا عَنْ عِبَادَتِكُمْ لَغَافِلِينَ ﴿٢٩﴾

29. Mwenyezi Mungu anatosha kuwa shahidi baina yetu na baina yenu. Hakika sisi tulikuwa hatuna habari ya ibada yenu.

Aya hizi zinabainisha jinsi hali itakavyokuwa siku ya Kiyama, ambapo Mwenyezi Mungu atawasimamisha mushirikina na wale waliokuwa wakiwaabudu na kuliuliza kila kundi peke yake; kwa nini nyinyi mlikuwa mkiyaabudu masanamu na miungu wa kubuni? Na nyinyi pia ilikuwaje mkaridhia kuabudiwa na watu hawa? Hapo ile miungu ya masanamu isiyo na uhai itapewa uhai kwa amri ya Mwenyezi Mungu na kuwakana wale waliokuwa wakiwaabudu na kutamka kuwa, "sisi hatukuwa tukijihesabu kuwa washirika wa Mwenyezi Mungu, bali nyinyi mlijitengenezea taswira akilini mwenu, na kuziabudu na sisi kutufanya kama kisingizio tu".

Aya ya 41 ya suratu Sabaa pia imeashiria maudhui hii na kueleza kuwa malaika nao ambao walikuwa wakiabudiwa wanadhihirisha, kuchukizwa kwao na kitendo hicho cha Mushrikina.

Nukta yenye mguso wa aina yake hapa ni kuwa katika aya hizi Allah s.w.t amewataja waabudiwa hao kuwa ni washirika wa Mushrikina kwa maana kwamba, hao hawakuwa waungu wanaoshirikishwa na Mwenyezi Mungu, bali ni washirika wenu nyinyi mushirikina mliojibunia na kujitengenezea wenyewe.

Miongoni mwa yale tunayojifunza katika aya hizi ni kuwa siku ya Kiyama, mbali ya wanaadamu, miungu na waabudiwa bandia yakiwemo masanamu yatapewa uhai ili kutoa ushahidi katika mahakama ya uadilifu dhidi ya mushirikina.

### AYA YA 30

Ifuatayo sasa ni aya ya 30 ambayo inasema:

هُنَالِكَ تَبْلُو كُلُّ نَفْسٍ مَّا أَسْلَفَتْ ۚ وَرُدُّوا إِلَى اللَّهِ مَوْلَاهُمُ الْحَقِّ ۖ وَضَلَّ عَنْهُم مَّا كَانُوا يَفْتَرُونَ ﴿٣٠﴾

30. Huko kila mtu atayajua aliyoyatanguliza. Na watarudishwa kwa Mwenyezi Mungu, Mola wao wa haki. Na yatawapotea yale waliyokuwa wakiyazua.

Baada ya masanamu na waabudiwa wengine kuwakana mushirkina, hapo makundi mawili hayo yatatenganishwa na mushirikina hawatoweza kuwaomba msaada hao waliokuwa wakiwafanya washirika wa Mwenyezi Mungu hapa duniani, na badala yake watarejea kwa Mola wao wa haki yaani Allah sw na hapo ndipo watapata jaza na malipo ya amali zao.

### AYA YA 31

Tunaiendeleza darsa yetu kwa aya ya 31 ambayo inasema:

قُلْ مَن يَرْزُقُكُم مِّنَ السَّمَاءِ وَالْأَرْضِ أَمَّن يَمْلِكُ السَّمْعَ وَالْأَبْصَارَ وَمَن يُخْرِجُ الْحَيَّ مِنَ
الْمَيِّتِ وَيُخْرِجُ الْمَيِّتَ مِنَ الْحَيِّ وَمَن يُدَبِّرُ الْأَمْرَ فَسَيَقُولُونَ اللَّهُ فَقُلْ أَفَلَا تَتَّقُونَ ﴿٣١﴾

31. Sema: 'Ni nani anayekuruzukuni kutoka mbinguni na katika ardhi. Au ni nani anayemiliki kusikia na kuona? Na ni nani amtoaye mzima katika mfu na kumtoa mfu katika mzima?Na nani anaye yadabiri mambo yote?' Watasema: 'Ni Mwenyezi Mungu.' Basi sema: 'Je Hamuogopi?

Baada ya aya zilizotangulia ambazo zimeonyesha unyonge na udhalili utakaowapata washirikina siku ya Kiyama, Mwenyezi Mungu anamwambia Mtume wake awaulize watu hao kuwa nyinyi ambao mnamkubali Mwenyezi Mungu, na mnajua kuwa ni yeye ndiye anayekuruzukuni, na ni yeye ndiye anayesimamia mambo yenu yote, kwa nini basi badala ya kumwabudu yeye mnayaabudu masanamu na kuyafanya wasita na waunganishi wa mambo yenu kwa Mwenyezi Mungu?

Kama ambavyo katika aya nyingine za quran imeelezwa kuwa mushirikina wa enzi za ujahiliya walikuwa wakikubali kuwa Mwenyezi Mungu ndiye Muumba wao na Muumba wa ulimwengu, ama katika suala la kuendesha mambo, mamlaka hayo yako mikonnoni mwa malaika na vitu vingine vya maumbile, kama kwamba Mwenyezi Mungu ameumba tu kisha akakaa kando na kulikabidhi kwa viumbe hao suala la uendeshaji wa ulimwengu.

Fikra ya aina hii imeelezwa na quran tukufu kuwa ni batili na aina mojawapo ya kumshirikisha Mwenyezi Mungu. Funzo mojawapo tunalopata katika aya hii ni kuwa uendeshaji wa ulimwengu unahitajia tadbiri isiyobadilika, na hili halingewezekana kama kungekuwepo na Muumba zaidi ya mmoja.

### AYA ZA 32 NA 33

Aya za 32 na 33 ndizo zinazotuhitimishia darsa yetu hii. Aya hizo zinasema:

فَذَٰلِكُمُ اللَّهُ رَبُّكُمُ الْحَقُّ فَمَاذَا بَعْدَ الْحَقِّ إِلَّا الضَّلَالُ فَأَنَّىٰ تُصْرَفُونَ ﴿٣٢﴾

32. Basi huyo ndiye Mwenyezi Mungu Mola wenu wa haki. Na kipo kitu gani baada ya haki isipokuwa upotofu tu? Basi huwaje mkageuzwa?

كَذَٰلِكَ حَقَّتْ كَلِمَتُ رَبِّكَ عَلَى الَّذِينَ فَسَقُوا أَنَّهُمْ لَا يُؤْمِنُونَ ﴿٣٣﴾

33. Hivi ndivyo kauli ya Mola wako itakavyowathubutikia wale walioasi, ya kwamba hawataamini.

Baada ya aya zilizotangulia kubainisha mifano ya ishara za adhama ya Mwenyezi Mungu katika uumbaji wa mbingu na ardhi pamoja na kukiri kwa washirikina kuhusu uumbaji wa Mwenyezi Mungu.

aya hizi zinabainisha wazi kuwa Mungu huyu ndiye Mola wenu, na vile vile ndiye muendeshaji mambo yenu; na si kwamba yeye ni muumba wenu lakini masanamu yakawa ndio waendeshaji wa mambo yenu.

Kisha aya zinaendelea kwa kutoa kauli ya mkato kwamba, hakuna hali ya tatu baada ya haki na batili. Kwa maana kwamba kila kitu ima ni haki au ni batili, na kwa hivyo kwa kuwa Mwenyezi azza wa jal ndiye haki, basi bila shaka masanamu na miungu wenu wengine wa kubuni hawawezi kuwa haki, na hivyo wale watu wanaoamua kuipa mgongo haki kwa inadi, ubishi na ukaidi hawawezi kupata taufiki ya kuufikia uongofu.

Baadhi ya yale tunayojifunza kutokana na aya hizi ni kuwa hakuna njia ya tatu baada ya haki na batili. Na kwa hivyo yanapothibitika mawili hayo, hakuna nafasi ya mtu kudai kuwa yeye hayuko huku wala huku bali ni mtu wa kati na kati.

Kwa haya machache tunaifunga darsa yetu hii. Tunamwomba Allah atuepushe na shirki na kuijenga imani kamili na safi ya tauhidi ndani ya nyoyo zetu. Amin

Wassalaamu Alaykum Warahmatullahi Wabarakaatuh.

## SURAT YUNUS 34-38

Tunamshukuru Mwenyezi Mungu mtukufu kwa kutuwafikisha kukutana tena katika darsa yetu hii.

### AYA ZA 34 NA 35

Sura ya 10 ya Yunus ndiyo tunayoizungumzia kwa sasa, na hii ni darsa ya 313 tunayoianza kwa aya za 34 na 35 ambazo zinasema:

قُلْ هَلْ مِن شُرَكَائِكُم مَّن يَبْدَأُ الْخَلْقَ ثُمَّ يُعِيدُهُ قُلِ اللَّهُ يَبْدَأُ الْخَلْقَ ثُمَّ يُعِيدُهُ فَأَنَّىٰ تُؤْفَكُونَ ﴿٣٤﴾

34. Sema: Je Yupo katika miungu yenu ya ushirikina, aliyeanzisha kuumba viumbe kisha akavirejesha? Sema: Mwenyezi Mungu ameanzisha kuumba viumbe kisha ndiye atakayevirejesha. Huwaje basi mkadanganywa?.

قُلْ هَلْ مِن شُرَكَائِكُم مَّن يَهْدِي إِلَى الْحَقِّ قُلِ اللَّهُ يَهْدِي لِلْحَقِّ أَفَمَن يَهْدِي إِلَى الْحَقِّ أَحَقُّ أَن يُتَّبَعَ أَمَّن لَّا يَهِدِّي إِلَّا أَن يُهْدَىٰ فَمَا لَكُمْ كَيْفَ تَحْكُمُونَ ﴿٣٥﴾

35. Sema: Je Yupo katika miugu yenu ya ushirikina anayeongoa kuendea Haki? Sema: Mwenyezi Mungu anaongoa kwendea Haki. Basi je anayestahiki kufuatwa ni yule Mwenye kuongoa kwendea Haki au asiyeongoa ila aongozwe yeye? Basi nyinyi mna nini? Mnahukumu namna gani?.

Zikiendelea kuzungumzia yale yaliyokuja katika aya zilizotangulia kuhusu kutoa changamoto kwa mushrikina ya kuwaonyesha jinsi miungu yao bandia isivyo na uwezo wa kufanya lolote, aya tulizosoma zinasema, ikiwa mtatupia jicho na kuzingatia uumbaji ulivyo mtabaini kuwa hakuna yeyote ghairi ya Mungu Mmoja awezaye kuumba kila kilichopo na kukipa uhai mpya, na hayo masanamu yenu mnayoyaabudu na viumbe vingine vyote vilivyoko, vyote hivyo vimeumbwa na vinamhitajia Muumbaji, basi yawaje vitu hivyo viweze navyo kuwa waumbaji wa ulimwengu?

Kama nyinyi ni wenye kutafuta uongofu na kutaka kuifikia saada tambueni kuwa miungu wenu hao wenyewe hawana cha kumuongoza mtu hata muweze kupata muongozo wa kufuata kutoka kwao, na kama ni suala la kupata uongofu, inalazimu wao wenyewe kwanza wawe na sifa hiyo ya kuweza kuufikia huo uongofu kisha ndipo waweze kukuonyesheni nyinyi pia njia ya kuufikia. Hali ya kuwa Mwenyezi Mungu ndiye muongozaji wenu wa kukufikisheni kwenye njia iliyonyooka. Tabaan uongofu wa Mwenyezi Mungu unapatikana kupitia Mitume wake na vitabu vya mbinguni walivyokuja navyo ambavyo kila kilichomo ndani yake ni maneno yake Mola Muumba.

Miongoni mwa yale tunayojifunza kutokana na aya hizi ni kuwa kutumia mfumo wa masuali na majibu ni mojawapo ya mbinu bora kwa ajili ya kujadiliana na wapinzani wa kiitikadi na kifikra, mbinu ambayo Allah sw amewafunza Mitume wake. Aidha aya zinatuelimisha kuwa Mwenyezi Mungu si Muumbaji wa ulimwengu tu, bali baada ya kuwaumba viumbe wake hakuwaacha kama walivyo, ila amewaonyesha pia njia yao ya uongofu itakayowafikisha kwenye saada ya duniani na akhera.

## AYA YA 36

Ifuatayo sasa ni aya ya 36 ambayo inasema:

وَمَا يَتَّبِعُ أَكْثَرُهُمْ إِلَّا ظَنًّا إِنَّ الظَّنَّ لَا يُغْنِي مِنَ الْحَقِّ شَيْئًا إِنَّ اللَّـهَ عَلِيمٌ بِمَا يَفْعَلُونَ ﴿٣٦﴾

36. Na wengi wao hawafuati ila dhana tu. Na dhana haifai kitu mbele ya haki. Hakika Mwenyezi Mungu anajua yote wanayoyatenda.

Aya hii wapenzi wasomaji inaashiria chanzo na chimbuko la upotofu wa kifikra la wale wanaomkanusha na kumkufuru Mwenyezi Mungu na kueleza kuwa kufuata dhana na mambo ya udhanifu yasiyo na msingi ambayo kwa hakika ni njozi za kifikra ndiyo yaliyowafanya watu hao waipe mgongo haki na kung'ang'ania fikra na itikadi batili.

Hali ya kuwa katika masuala ya kifkra na kiitikadi, dhana na mambo ya udhanifu hayana nafasi wala itibari yoyote, na ukweli ni kuwa hakika na yakini ndiyo mambo yanayoweza kumfikisha mtu kwenye haki.

Mbali na hayo chimbuko la itikadi nyingi za zama za ujahilia lilikuwa ni watu kufuata yale waliyowakuta nayo babu zao na kushikilia na kuyanng'ang'ania mambo kwa sababu ya taasubi tu za kikabila, mambo ambayo hayakuwa na thamani wala itibari yoyote ya kielimu na kifikra.

Baadhi ya yale tunayojifunza kutokana na aya hii ni kuwa katika masuala ya kiitikadi na kimaadili wingi hauwi kipimo cha kuonyesha haki. Kwani si hasha walio wengi katika watu wakawa wamepotoka kifikra na kimatendo.

## AYA ZA 37 NA 38

Tunaihitimisha darsa yetu ya juma hili kwa aya za 37 na 38 ambazo zinasema:

وَمَا كَانَ هَـٰذَا الْقُرْآنُ أَن يُفْتَرَىٰ مِن دُ    ونِ اللَّـهِ وَلَـٰكِن تَصْدِيقَ الَّذِي بَيْنَ يَدَيْهِ وَتَفْصِيلَ

الْكِتَابِ لَا رَيْبَ فِيهِ مِن رَّبِّ الْعَالَمِينَ ﴿٣٧﴾

37. Na haiwezekani Qurani hii kuwa imetungwa, na haitoki kwa Mwenyezi Mungu. Bali inayasidikisha yaliyotangulia, na ni mfafanuo wa Kitabu kisicho na shaka ndani yake kutoka kwa Mola wa walimwengu wote.

أَمْ يَقُولُونَ افْتَرَاهُ ۖ قُلْ فَأْتُوا بِسُورَةٍ مِّثْلِهِ وَادْعُوا مَنِ اسْتَطَعْتُم مِّن دُونِ اللَّـهِ إِن كُنتُمْ صَادِقِينَ ﴿٣٨﴾

38. Je! Ndiyo wanasema ameizua? Sema:" Hebu leteni sura moja mfano wake na muwaite (kukusaidieni) muwawezao isipokuwa Mwenyezi Mungu ikiwa nyinyi mnasema kweli.

Quran tukufu imetoa changamoto mara kadhaa ya kuthibitisha kuwa ni maneno ya mbinguni na kuonyesha kwamba si majini wala binaadamu walio na uwezo wa kuleta kitu kilicho mfano wake.

Bali ikafika mbali zaidi na kueleza kwa kujiamini kwamba, si kuleta mfano wa Quran yote au moja ya sura zake tu, bali kama wana uwezo, wapinzani wa muujiza huo wa Mtume wa mwisho wa Mwenyezi Mungu na walete walau aya moja tu iliyo mfano wa Quran.

Hata hivyo licha ya maadui na wapinzani wengi ambao Uislamu na Quran imekabiliana nao katika kipindi cha karne 14 zilizopita, hadi leo hii hakuna aliyethubutu kujitokeza kukabiliana na changamoto hiyo iliyotolewa na kitabu hicho cha Mwenyezi Mungu.

Magwiji wa kila zama wa nahau na balagha pamoja na fani nyinginezo za lugha ya kiarabu wasio waislamu, wote hao wameshindwa kubuni walau aya moja tu iliyo na sifa za aya ya Quran tukufu.

Wapenzi wasomaji quran tukufu ina miujiza na maajabu ya aina kwa aina, machache kati ya hayo ni haya yafuatayo:

**Kwanza**: ni utamu wa maneno yake na mvuto wa ajabu yalionao, kiasi kwamba hata kama mtu ataisoma mara elfu hahisi kuwa amesoma kitu cha kushosha na kilichopitwa na wakati. Si hayo tu, bali vibwagizo vya maneno yake, mianguko yake ya sauti na mahadhi yake yamejipambanua na maneno mengine yote ya lugha ya kiarabu.

Ujumuishaji wa quran wa kila kipengele cha maisha ya mwanadamu vikiwemo vya masuala ya mtu binafsi, familia, jamii, masuala ya kisheria, kiuchumi, kisiasa na kiakhalqi ni wa namna ambayo, ni muhali kwa mwanaadamu yeyote kuweza kuufikia upeo wake.

Wapenzi wasomaji darsa ya 313 imefikia tamati. Tunamwomba Mwenyezi Mungu aturuzuku kuisoma quran usiku na mchana, kwa namna airidhiayo yeye, na kutuwafikisha kutekeleza kivitendo yaliyomo ndani yake ili tuweze kupata uombezi wa quran siku ya kiyama. Amin.

Wassalaamu Alaykum Warahmatullahi Wabarakaatuh.

## SURAT YUNUS 39-44

Assalaamu Alaykum Warahmatullahi Wabarakaatuh.

Karibuni katika mfululizo huu wa 314 wa darsa ya quran, tukiwa tunaendelea kuizungumzia sura ya 10 ya Yunus.

### AYA ZA 39 NA 40

Tunaianza darsa yetu kwa aya za 39 na 40 ambazo zinasema:

بَلْ كَذَّبُوا بِمَا لَمْ يُحِيطُوا بِعِلْمِهِ وَلَمَّا يَأْتِهِمْ تَأْوِيلُهُ ۚ كَذَٰلِكَ كَذَّبَ الَّذِينَ مِن قَبْلِهِمْ ۖ فَانظُرْ كَيْفَ كَانَ عَاقِبَةُ الظَّالِمِينَ ﴿٣٩﴾

39. Bali wameyakanusha wasiyoyaelewa ilimu yake kabla hayajawajia maelezo yake. Namna hivi walikanusha waliokuwa kabla yao. Basi angalia jinsi ulivyokuwa mwisho wa madhalimu hao.

وَمِنْهُم مَّن يُؤْمِنُ بِهِ وَمِنْهُم مَّن لَّا يُؤْمِنُ بِهِ ۚ وَرَبُّكَ أَعْلَمُ بِالْمُفْسِدِينَ ﴿٤٠﴾

40. Na miongoni mwao wapo wanaoiamini. Na miongoni mwao wapo wasioiamini. Na Mola wako anawajua vyema waharibifu.

Katika darsa iliyopita tulisema kuwa kutokana na dhana tu na bila kuwa na ushahidi mushirikina na makafiri walikuwa walivurumiza tuhuma kuwa Quran ni maneno ya Bwana Mtume na kukanusha kwa kudai kuwa kitabu hicho kitukufu hakina uhusiano wowote na Mwenyezi Mungu.

Aya tulizosoma zinasema kuwa kinachofanywa na makafiri na mushirikina hao ni kukariri yale yaliyosemwa na wenzao waliotangulia, kwani mitume wa kabla ya Nabii Muhammad **(s.a.w.w)** walikabiliwa na tuhuma sawa na hizo.

Hii ni pamoja na kuwa ukadhibishaji wao hauna mashiko yoyote ya kielimu, hivyo kitendo chao hicho ni sawa na kujidhulumu nafsi zao na pia ni dhulma kwa dini ya haki ya mbinguni na mitume waliotumwa na Allah kuitangaza dini hiyo kwa watu.

Lakini katika upande mwingine, kuna watu wanaoitambua na kuiamini haki, na hivyo, kama tulivyowahi kuashiria mara kadhaa, ndivyo alivyokadiria Allah s.w.t, kwamba: kila mtu kwa hiyari mwenyewe aamue ima kuwa muumini au kafiri. Baadhi ya yale tunayojifunza kutokana na aya hizi ni kuwa chanzo cha ukafiri, ukanushaji na ukadhibishaji haki ni kukosa utambuzi wa kuielewa haki hiyo. Kwani wale wanaokusudia kwa dhati kuitafuta na kutaka kuijua haki hufika mahali wakaitambua risala ya tauhidi waliyokuja nayo Mitume wa Mwenyezi Mungu na wakaiamni.

Aidha aya zinatuelimisha kuwa kuyakanusha na kuyapa mgongo mafundisho ya manabii wa Allah ndiyo chanzo cha dhulma na ufisadi tunaoushuhudia ulimwenguni.

## AYA YA 41

Ifuatayo sasa ni aya ya 41 ambayo inasema:

وَإِن كَذَّبُوكَ فَقُل لِّي عَمَلِي وَلَكُمْ عَمَلُكُمْ ۖ أَنتُم بَرِيئُونَ مِمَّا أَعْمَلُ وَأَنَا بَرِيءٌ مِّمَّا تَعْمَلُونَ

﴿٤١﴾

41. Na wakiendelea kukukadhibisha sema: Mimi nina amali yangu na nyinyi mna amali yenu. Nyinyi hamna dhima kwa niyatendayo, wala mimi sina dhima kwa mnayotenda nyinyi.

Aya hii inabainisha jinsi ya kuamiliana na makafiri na wapinzani wa haki na kueleza kuwa jukumu lenu nyinyi kwa watu hao ni kuwaonyesha tu na kuwatambulisha uongofu; si kuwalazimisha wao waufuate kwa nguvu, wala nyinyi kutaka kuwakumbatia wao ili kiwe kishawishi cha kuwafanya wavutiwe na haki.

Ikiwa wao watakuwa wamekaidi na kukataa kata kata kuiamini haki, dhima yenu kwao imeshaondoka, kwani imani ni jambo la moyoni na la hiyari, na hivyo watu hao ni kwamba wameshaamua hawataki kuielewa haki, na kama wameielewa, basi hawataki kuiamini.

Katika suala hili hutokezea baadhi ya Waislamu wakahisi kuwa labda ikiwa wao wenyewe wataamua kuacha kushikamana na baadhi ya mambo ya msingi ya dini huenda hilo linaweza kuwavutia wale wanaowalingania waikubali haki. Hali ya kuwa mtu hana haki yoyote ya kufanya hivyo kwa sababu tu ya kutaka kupata idadi kubwa zaidi ya watu walioukubali uongofu.

Na ndiyo maana tunaona katika aya hizi Bwana Mtume Muhammad saw anatakiwa awaambie makafiri kwamba, madamu nyinyi hamko tayari kuyaamini maneno yangu, tambueni kuwa mimi najiweka mbali kabisa na matendo yenu na wala sina dhima wala jukumu lolote kwenu.

Funzo mojawapo tunalolipata katika aya hii ni kuwa Uislamu ni dini ya hoja, maadili na msimamo. Inatangaza na kuweka wazi msimamo wake; na kama ambavyo haimlazimishi mtu kuifuata, ndivyo vivyo hivyo nayo haiko tayari kulegeza msimamo katika misingi ya mafundisho yake.

## AYA ZA 42, 43 NA 44

Darsa ya 314 inahitimishwa na aya za 42, 43 na 44 ambazo zinasema:

وَمِنْهُم مَّن يَسْتَمِعُونَ إِلَيْكَ ۚ أَفَأَنتَ تُسْمِعُ الصُّمَّ وَلَوْ كَانُوا لَا يَعْقِلُونَ ﴿٤٢﴾

42. Na wako miongoni mwao wanaokusikiliza. Je wewe unaweza kuwafanya viziwi wasikie ijapokuwa hawafahamu?.

وَمِنْهُم مَّن يَنظُرُ إِلَيْكَ ۚ أَفَأَنتَ تَهْدِي الْعُمْيَ وَلَوْ كَانُوا لَا يُبْصِرُونَ ﴿٤٣﴾

43. Na wapo miongoni mwao wanaokukodolea macho. Je wewe utawaongoa vipofu ingawa hawaoni?

إِنَّ اللَّـهَ لَا يَظْلِمُ النَّاسَ شَيْئًا وَلَـٰكِنَّ النَّاسَ أَنفُسَهُمْ يَظْلِمُونَ ﴿٤٤﴾

44. Hakika Mwenyezi Mungu hawadhulumu watu chochote; lakini watu wenyewe wanajidhulumu nafsi zao.

Katika kuendeleza yale yaliyokuja katika aya zilizotangulia kuhusu jinsi wapinzani wa haki walivyokuwa wakiamiliana na Bwana Mtume, aya hizi zinasema, si hasha baadhi ya wapinzani hao wakawa ni watu wanaohudhuria vikao vya Bwana Mtume, wakimwona kwa macho yao mtukufu huyo na kuyasikia yale anayoyasema; lakini yote hayo hayazipi athari yoyote nafsi zao. Na sababu ni kuwa yote hayo waliyokuwa wakiyashuhudia na kuyasikia hayakuwa yakipenya kweli kwenye masikio yao na kukita kwenye fikra na nyoyo zao.

Kana kwamba watu hao walikuwa ni vipofu wasioona au viziwi wasioweza kusikia chochote. Kimsingi ni kwamba kitu kinachompambanua mwanadamu na mnyama ni uwezo wake wa kufikiri na kutafakari, vinginevyo mnyama naye anaona na anasikia, bali hata uwezo na nguvu zake zake za kuona na kusikia ni kubwa zaidi kuliko za binaadamu. Hivyo linalomstahikia mwanadamu ni kuyatia kwenye tafakuri yale ayaonayo na ayasikiayo, kwa kupambanua la haki na la batili, kisha kushikamana na lile la haki na kujiweka mbali na lile la batili. Funzo mojawapo tunalolipata kutokana na aya hizi ni kuwa kuona na kusikia, ni utangulizi wa kutafakari na kuifahamu haki.

Wapenzi wasomaji darsa yetu ya juma hili inaishia hapa. Tunamwomba Allah atuwafikishe kuitambua haki na kuifuata, na kuielewa batili na kuiepuka. Amin.

Wassalaamu Alaykum Warahmatullahi Wabarakaatuh.

## SURAT YUNUS 45-49

Tunamshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa kutuwafikisha kukutana tena katika darsa yetu hii.

### AYA YA 45

Sura ya 10 ya Yunus ndiyo tunayoizungumzia kwa sasa, na hii ni darsa ya 315 tunayoianza kwa aya ya 45 ambayo inasema:

وَيَوْمَ يَحْشُرُهُمْ كَأَن لَّمْ يَلْبَثُوا إِلَّا سَاعَةً مِّنَ النَّهَارِ يَتَعَارَفُونَ بَيْنَهُمْ قَدْ خَسِرَ الَّذِينَ كَذَّبُوا بِلِقَاءِ اللَّـهِ وَمَا كَانُوا مُهْتَدِينَ ﴿٤٥﴾

45. Na siku atakapowakusanya, itakuwa kama kwamba hawakukaa (duniani) ila saa moja tu ya mchana. Watatambuana. Hakika wamekhasirika wale waliokanusha kukutana na Mwenyezi Mungu, wala hawakuwa wenye kuongoka.

Ijapokuwa makafiri wamekadhibisha na kukanusha kuwepo kwa siku ya kiyama, hata hivyo watake wasitake ni kwamba wao pia kama ilivyo kwa wanaadamu wote watafufuliwa tu na kuishuhudia siku hiyo.

Uzito wa siku hiyo utakuwa hauna mfano wake kiasi cha kuwafanya wale waliokufuru wahisi kwamba umri wao wote walioishi hapa duniani, pamoja na kipindi chote cha maisha ya barzakh huko makaburini, ulikuwa ni sawa na muda wa saa moja tu ya mchana mzima.

Pamoja na wanaadamu kupitiwa na miaka bali pengine karne nyingi za baada ya kufa kwao, lakini watahisi kana kwamba wameamka tu kutoka kwenye usingizi wa kawaida. Katika hali hiyo watu watatambuana vizuri na wala hawatokumbwa na usahaulifu.

Ni wazi kwamba katika lahadha hiyo wale ambao hapa duniani walikanusha kuwepo kwa kiyama, wakati kweli itakapodhihiri na kujiona wamesimamishwa katika uwanja wa siku ya kiyama, hapo ndipo watakapobaini kuwa wao ni watu waliokhasirika kwa kufika mahala hapo wakiwa mikono mitupu, huku kukiwa hakuna tena fursa ya kurudi walikotoka.

Baadhi ya mafunzo tunayopata kutokana na aya hii ni kuwa umri tunaoishi hapa duniani ni mfupi, kiasi kwamba siku ya kiyama mtu atajuta na kujihisi amekhasirika na kupata hasara kubwa kwa kutoitumia fursa hiyo ya uhai wa kupita aliojaaliwa hapa duniani.

Halikadhalika inatubainikia kutokana na aya hii ni kuwa hasara ya kweli ni ile ya mtu kuhitari na kufadhilisha starehe za kupita za hapa duniani kwa raha na neema za milele za huko akhera.

### AYA YA 46

Tunaiendeleza darsa yetu kwa aya ya 46 ambayo inasema:

وَإِمَّا نُرِيَنَّكَ بَعْضَ الَّذِي نَعِدُهُمْ أَوْ نَتَوَفَّيَنَّكَ فَإِلَيْنَا مَرْجِعُهُمْ ثُمَّ اللَّـهُ شَهِيدٌ عَلَىٰ مَ ا يَفْعَلُونَ ﴿٤٦﴾

46. Na vyovyote vile, tukikuonyesha baadhi ya tunayowaahidi au tukakufisha kabla yake, marejeo yao ni kwetu. Kisha Mwenyezi Mungu ni shahidi wa wanayoyafanya.

Aya hii inamliwaza Bwana Mtume na waumini kwa kuwaambia kuwa ikiwa mnaona Mwenyezi Mungu hawashushii adhabu kamili makafiri hapa duniani ni kwa sababu malipo hasa ya waja iwe ni adhabu ya moto au neema ya pepo wataipata huko akhera pale wote watakaporejea kwa Mola wao.

Hata hivyo sio kwamba adhabu ya kila ovu itasubiri huko akhera tu bali baadhi ya adhabu zitawashukia wakanushaji hapo papa hapa duniani, nawe Mtume utashuhudia kwa macho yako; na baadhi ya adhabu zitawashukia hata baada ya wewe kuaga dunia.

Funzo mojawapo tunalopata katika aya hii ni kuwa waislamu wasikate tamaa kuona muda unapita bila makafiri kupatwa na adhabu ya Mwenyezi Mungu.

Hiyo ni ahadi ya Mwenyezi Mungu, na Mwenyezi Mungu ni mtimizaji wa ahadi anayotoa, tabaan kulingana na hikima yake mutlaki.

### AYA YA 47

Ifuatayo sasa ni aya ya 47 ambayo inasema:

وَلِكُلِّ أُمَّةٍ رَّسُولٌ فَإِذَا جَاءَ رَسُولُهُمْ قُضِيَ بَيْنَهُم بِالْقِسْطِ وَهُمْ لَا يُظْلَمُونَ ﴿٤٧﴾

47. Na kila umma una Mtume. Alipowajia Mtume wao walihuhukumiwa baina yao kwa uadilifu; wala hawakudhulumiwa.

Mitume wa Mwenyezi Mungu walikuwa katika makundi mawili. Wale waliopewa vitabu na sheria, na wale ambao walikuwa wafikishaji na walinganiaji tu wa risala za Mitume waliopewa vitabu na sheria. Kutokana na aya za quran inabainika kuwa katika kipindi cha historia, na katika umma na kaumu mbali mbali za wanaadamu wamekuwepo watu waliokuwa wakiwafikishia wanadamu wenzao mafundisho ya mitume na yale yaliyokuja katika vitabu vya mbinguni.

Na ujumbe mkuu katika risala za manabii ulikuwa ni kusimamisha haki na uadilifu na kupambana na dhulma na uonevu. Na hivyo siku ya kiyama Allah sw ataawafufua watu wa kila kaumu na umati pamoja na Mtume wao na kuwasimamisha na kuwahukumu kwa uadilifu katika mahakama ya siku hiyo ya malipo.

Funzo mojawapo tunalopata kutokana na aya hii ni kuwa: hakuna uma au kaumu yoyote ambayo Mwenyezi Mungu ameiwacha vivi hivi bila ya kuhakikisha imefikiwa na ujumbe wa mafundisho ya Mitume wake.

### AYA ZA 48 NA NA 49

Tunaihitimisha darsa yetu kwa aya za 48 na na 49 ambazo zinasema:

وَيَقُولُونَ مَتَىٰ هَـٰذَا الْوَعْدُ إِن كُنتُمْ صَادِقِينَ ﴿٤٨﴾

48. Na wanasema: Ni lini ahadi hii ikiwa mnasema kweli?

قُل لَّا أَمْلِكُ لِنَفْسِي ضَرًّا وَلَا نَفْعًا إِلَّا مَا شَاءَ اللَّـهُ لِكُلِّ أُمَّةٍ أَجَلٌ إِذَا جَاءَ أَجَلُهُمْ فَلَا يَسْتَأْخِرُونَ سَاعَةً وَلَا يَسْتَقْدِمُونَ ﴿٤٩﴾

49. Sema: Sijimilikii nafsi yangu shari wala kheri, ila apendavyo Mwenyezi Mungu. Kila umma una muda wao waliowekewa. Ukifika muda wao hawakawii saa moja wala hawatangulii.

Makafiri ambao waliamua kukanusha hakika ya kuwepo kwa siku ya kiyama waliamua kuzusha visingizio vya kila aina alimradi kuutia shaka uhakika huo.

Hivyo wakaibuka na suali kwamba ikiwa ni kweli kiyama kitatokea na wewe Muhammad unayoyasema ni kweli kuhusu hilo, tuambie basi kujiri kwake kutakuwa lini hasa! Walizusha hoja hiyo ilhali uhakika wa kutokea jambo haushurutishi kujua wakati halisi wa kutokea kwake. Mfano wa hili ni sawa na mauti.

Kila mmoja wetu ana hakika kuwa iko siku ataiaga dunia tu, lakini hakuna yeyote kati yetu ajuaye ni lini hasa atafikwa na mauti. Kwa upande wa Bwana Mtume, naye pia kupitia wahyi alioushushiwa na Mola wake aliwapa khabari watu wa umati wake kwamba baada ya kumalizika dunia itawadia siku ya Kiyama, hata hivyo Allah s.w.t hakumbainishia Mtume wake ni wakati gani hasa litajiri tukio hilo kubwa kabisa la kutikisa nyoyo.

Baadhi ya mafunzo tunayoyapata kutokana na aya hizi ni kuwa Mitume walikuwa ni waja wateule wanaozungumza na watu kwa uwazi na ukweli mtupu; na hivyo wakiwaeleza bayana kuwa binafsi hawana nguvu na uwezo usio wa kawaida wala mamlaka ya kujiamulia kupata manufaa fulani au kujilinda na kujiepusha na shari yoyote ile ila kwa uwezo na idhini ya Allah s.w.t

Wapenzi wasomaji, kwa haya machache tunaifunga darsa hii ya 315. Inshaallah Mwenyezi Mungu atujaalie kuwa miongoni mwa wanaoyakinisha kiimani juu ya kuwepo kwa siku ya kiyama kutokana na amali zao na matendo yao.

Wassalaamu Alaykum Warahmatullahi Wabarakaatuh

4

# TAFSIRI YA SUURAT YUUNUS

## SURAT YUNUS 50-56

Bismillahir Rahmanir Rahim. Assalaamu Alaykum Warahmatullahi Wabarakaatuh.

Karibuni katika mfululizo huu wa 316 wa darsa la quran, tukiwa tunaendelea kuizungumzia sura ya 10 ya Yunus.

### AYA ZA 50 NA 51

Tunaianza darsa yetu kwa aya za 50 na 51 ambazo zinasema:

قُلْ أَرَأَيْتُمْ إِنْ أَتَاكُمْ عَذَابُهُ بَيَاتًا أَوْ نَهَارًا مَّاذَا يَسْتَعْجِلُ مِنْهُ الْمُجْرِمُونَ ﴿٥٠﴾

50. Sema: Mwaonaje ikikufikieni hiyo adhabu yake usiku au mchana, basi kwa nini wenye makosa wanaitake ije haraka?

أَثُمَّ إِذَا مَا وَقَعَ آمَنتُم بِهِ آلْآنَ وَقَدْ كُنتُم بِهِ تَسْتَعْجِلُونَ ﴿٥١﴾

51. Tena Je! Ikishatokea mtaiamini? Ndio sasa tena? Na nyinyi mlikuwa mkiihimiza.

Aya hizi zinatoa jibu kwa wale wanaokanusha kufufuliwa kwa viumbe ambao walikuwa wakisema, hiyo adhabu ya Mwenyezi Mungu itatokea lini? Ndipo Bwana Mtume akatakiwa awajibu kuwa hivi nyinyi mnaoharakisha mteremshiwe adhabu, kama adhabu hiyo itakushukieni ghafla iwe ni mchana au pengine usiku mkiwa mmelala, mtafanya nini wakati huo? Je mtaweza kupata pa kukimbilia au kuwa na nguvu za kuizuia isikupateni? Kama mnadhani pia kwamba ikiwa mtaiamini haki pale mtakapoanza kuona ishara za kuteremka adhabu na kuwa imani yenu hiyo itaweza kukufaeni, basi dhana yenu hiyo ni batili, kwani pale itakaposhuka adhabu milango ya toba itafungwa na hivyo imani katika lahadha hiyo haitokuwa na taathira yoyote.

Miongoni mwa mafunzo tunayopata kutokana na aya hizi ni kuwa kuamini mtu wakati hatari iko mbele ya macho yake hakuna thamani yoyote, kwani imani ya aina hiyo si ya hiyari wala ya kuitakidiwa moyoni, bali ni imani inayotokana na khofu ya lisilo budi.

### AYA YA 52

Ifuatayo sasa ni aya ya 52 ambayo inasema:

ثُمَّ قِيلَ لِلَّذِينَ ظَلَمُوا ذُوقُوا عَذَابَ الْخُلْدِ هَلْ تُجْزَوْنَ إِلَّا بِمَا كُنتُمْ تَكْسِبُونَ ﴿٥٢﴾

52. Kisha waliodhulumu wataambiwa: Onjeni adhabu ya kudumu. Kwani mtalipwa isipokuwa yale mliyokuwa mkiyachuma?

Katika aya zilizotangulia lilizungumziwa suala la adhabu ya Mwenyezi Mungu ya hapa duniani inayowashukia kwa ghafla waovu na waliomkufuru Mola Aliyetukuka.

Aya hii ya 52 inaashiria adhabu ya milele itakayowapata waovu hao siku ya Kiyama kwa sababu ya dhulma waliojitendea wao wenyewe na kuwatendea wanadamu wenzao.

Baadhi ya mafunzo tunayoyapata kutokana na aya hii ni kuwa katika mafundisho ya Uislamu mpaka wa dhulma hauishii katika kutenda dhulma kwa wengine tu, lakini hata madhambi anayoyafanya yeye mwenyewe mtu

yanahesabika pia kuwa ni dhulma, kwani ufanyaji dhambi huo ni sawa na mtu kujidhulumu nafsi yake na pia kuwafanyia dhulma Mitume wa Allah ambao walitaabika na kupata mashaka mengi kwa ajili ya kuhakikisha uongofu utokao kwa Allah unawafikia waja wake.

Aidha aya inatuelimisha kuwa adhabu ya Mwenyezi Mungu itakuwa ya kiadilifu kulingana na amali zake mwenyewe mja, bila kuzidishiwa kitu.

### AYA ZA 53 NA 54

Tunaiendeleza darsa yetu kwa aya za 53 na 54 ambazo zinasema:

وَيَسْتَنبِئُونَكَ أَحَقٌّ هُوَ قُلْ إِي وَرَبِّي إِنَّهُ لَحَقٌّ وَمَا أَنتُم بِمُعْجِزِينَ ﴿٥٣﴾

53. Na wanakuuliza: Je! ni kweli hayo? Sema: Ehe! Naapa kwa Mola wangu! Hakika hayo ni kweli nanyi hamuwezi kumshinda (Mwenyezi Mungu).

وَلَوْ أَنَّ لِكُلِّ نَفْسٍ ظَلَمَتْ مَا فِي الْأَرْضِ لَافْتَدَتْ بِهِ وَأَسَرُّوا النَّدَامَةَ لَمَّا رَأَوُا الْعَذَابَ وَقُضِيَ بَيْنَهُم بِالْقِسْطِ وَهُمْ لَا يُظْلَمُونَ ﴿٥٤﴾

54. Na lau kuwa kila nafsi iliyodhulumu inamiliki kila kilichomo duniani, bila shaka ingelitoa vyote kujikombolea. Na watakapoiona adhabu watajitahidi kuficha majuto yao. Na patahukumiwa baina yao kwa uadilifu nao hawatodhulumiwa.

Baada ya aya zilizotangulia kuelezea juu ya ushukaji wa adhabu ya Allah kwa waovu hapa duniani na ile itakayowapata huko akhera, aya hizi zinasema musiwe na shaka yoyote juu ya kushuka kwa adhabu ya Mwenyezi Mungu, kwani ahadi ya Mola itathibiti tu. Pamoja na kwamba yote aliyokuwa akiyatamka Bwana Mtume Muhammad **(s.a.w.w)** yalikuwa ni hakika na kweli tupu, lakini kutokana na uzito wa suala la kufufuliwa viumbe, hapa anaapa kwa jina la Mola Mwenyezi kuthibitisha kwamba kujiri kwa siku hiyo ya Kiyama hakuna chembe ya shaka, na wala hakuna atakayeweza kuikwepa siku hiyo au kuweza kukabiliana na adhabu yake.

Kwa hakika adhabu ya Mwenyezi Mungu siku ya Kiyama itakuwa kali na nzito kiasi kwamba, kila muovu atakuwa tayari kutoa mali na utajiri wote uliopo duniani ili aweze kuokoka na adhabu hiyo.

Lakini hiyo itabaki kuwa ni ya laiti ambayo haileti, kwa sababu kujuta wakati huo kwa yale aliyoyatanguliza mtu hakutosaidia kitu kwani mahakama ya Mwenyezi Mungu itatoa na kutekeleza hukumu kwa waja wote kwa msingi wa uadilifu.

Funzo mojawapo tunalolipata kutokana na aya hizi ni kuwa katika mahakama ya Mwenyezi Mungu si utajiri wala nguvu na uwezo wa kidunia vitakavyoweza kumsaidia mtu. Ni imani safi na sahihi, na amali njema zilizofanywa kwa ikhlasi, ndivyo vitakamvyomfaa mja siku hiyo.

### AYA ZA 55 NA 56

Darsa hii ya 316 nahitimishwa na aya za 55 na 56 ambazo zinasema:

أَلَا إِنَّ لِلَّـهِ مَا فِي السَّمَاوَاتِ وَالْأَرْضِ أَلَا إِنَّ وَعْدَ اللَّـهِ حَقٌّ وَلَـٰكِنَّ أَكْثَرَهُمْ لَا يَعْلَمُونَ ﴿٥٥﴾

55. Jueni kuwa hakika vyote vilivyomo katika mbingu na katika ardhi ni vya Mwenyezi Mungu. Jueni kuwa hakika ahadi ya Mwenyezi Mungu ni ya haki. Lakini wengi wao hawajui.

هُوَ يُحْيِي وَيُمِيتُ وَإِلَيْهِ تُرْجَعُونَ ﴿٥٦﴾

56. Yeye ndiye anayefufua na anayefisha. Na kwake mtarejeshwa.

Sababu kuu inayowafanya wanaokufuru na kukanusha juu ya kuwepo kwa siku ya Kiyama ni shaka yao juu ya uwezo wa Allah s.w.t Hivyo aya tulizosoma zinasema kuwa ni nini ikakupitikieni kwamba Mwenyezi Mungu hana uwezo wa kuwafufua waliokufa na kuwalipa kwa waliyotenda? Kwani hamujui nyinyi kuwa kila kitu ni milki yake yeye, na yeye ndiye Muumba na Mmiliki wa ulimwengu, na kwamba uhai wenu na mauti yenu viko mikononi mwake yeye? Kama mnayakubali hayo, yawaje basi mnakuwa na shaka juu ya kiyama?

Aya hizi wapenzi wasomaji zinatuelimisha kuwa mmiliki halisi wa kila kitu ni Mwenyezi Mungu s.w.t, na umiliki wa wanaadamu kwa kitu chochote kile ni wa kupanga tu. Na ndiyo maana siku ya kiyama wale waliokufuru hawatokuwa na chochote cha kuweza kutoa kama fidia ili waweze kuokoka.

Aidha aya zinatuonyesha kuwa uwezo wa Allah wa kutawala kila kitu ni ithbati tosha ya uwezo wake wa kutekeleza kila anachoahidi. Kwa haya machache tunaifunga darsa yetu hii huku tunamwomba Mola atujaalie kuwa miongoni mwa wale watakaopata radhi zake na pepo ya milele, na atulinde na ghadhabu zake na adhabu ya moto, amin

Wassalaamu Alaykum Warahmatullahi Wabarakaatuh.

## SURAT YUNUS 57-61

Tunamshukuru Mwenyezi Mungu mtukufu kwa kutuwafikisha kukutana tena katika darsa yetu hii.

### AYA ZA 57 NA 58

Sura ya 10 ya Yunus ndiyo tunayoizungumzia kwa sasa, na hii ni darsa ya 317 tunayoianza kwa aya za 57 na 58 ambazo zinasema:

يَا أَيُّهَا النَّاسُ قَدْ جَاءَتْكُم مَّوْعِظَةٌ مِّن رَّبِّكُمْ وَشِفَاءٌ لِّمَا فِي الصُّدُورِ وَهُدًى وَرَحْمَةٌ لِّلْمُؤْمِنِينَ ﴿٥٧﴾

57. Enyi watu Yamekujieni mawaidha kutoka kwa Mola wenu, na poza kuponyesha yaliyomo vifuani, na uwongofu, na rehema kwa waumini.

قُلْ بِفَضْلِ اللَّـهِ وَبِرَحْمَتِهِ فَبِذَٰلِكَ فَلْيَفْرَحُوا هُوَ خَيْرٌ مِّمَّا يَجْمَعُونَ ﴿٥٨﴾

Sema: Kwa fadhila ya Mwenyezi Mungu na rehma yake! Basi nawafurahi kwa hayo. Haya ni bora kuliko hayo wanayoyakusanya.

Roho ya mwanadamu wapenzi wasomaji kama ulivyo mwili wake huzongwa na mashaka na magonjwa mbali mbali ya kinafsi na hivyo nayo pia huhitajia dawa. Maradhi ya kiroho kama vile kiburi, ghururi, ubakhili, uhasidi na riya, kama hayatopatiwa dawa huweza kumfanya mtu aishie kwenye ukafiri na unafiki na kumtoa kwenye njia ya uongofu.

Na kwa hivyo quran kutokana na mawaidha na maonyo yake ya mara kwa mara huweza kumkinga mtu na kumwezesha kuepuka madhambi mbali mbali. Kwa upande mwingine kwa kubainisha adhabu iliyoandaliwa na

Mwenyezi Mungu kwa ajili ya waovu, kitabu hicho cha mbinguni humzindua na kumtanabahisha mwanadamu na matendo yake maovu ili achukue hatua ya kuisafisha na kuitakasa roho yake. Ni wazi kwamba nafsi zilizo safi ndizo zinazoweza kupata taufiki ya kuufikia uongofu wa Allah (s.w.t).

Hivyo Mola Mwenyezi anamtaka Mtume wake awaeleze waumini kwamba rasilimali bora kabisa kwao ni hiyo imani yao kwa kitabu cha Allah na kushikamana kwao na kitabu hicho, na kwa kweli wana kila sababu ya kufurahia kupata neema hiyo kubwa na si kupaparikia vyeo na utajiri wa kidunia.

Baadhi ya mafunzo tunayopata kutokana na aya hizi ni kuwa quran ndiyo ponya na dawa bora kabisa kwa nyoyo zenye maradhi na nafsi zilizo chafu kimaadili.

Aidha kutokana na aya hizi tunabaini kuwa quran ndiyo hazina na kito chenye thamani kubwa zaidi kuliko utajiri wa aina yoyote ile wa kidunia. Kwa hakika fukara hasa ni yule mtu aliyekosa mafundisho matukufu ya kitabu hicho, hata kama atakuwa amejikusanyia mali na kila aina ya utajiri.

Na kinyume chake tajiri na aliye mkwasi hasa ni yule anayeishi maisha ya kiquran hata kama kwa mtazamo wa kimaada na kidhahiri hatokuwa na mali wala utajiri wowote.

### AYA ZA 59 NA 60

Tunaiendeleza darsa yetu kwa aya za 59 na 60 ambazo zinasema:

قُلْ أَرَأَيْتُم مَّا أَنزَلَ اللَّـهُ لَكُم مِّن رِّزْقٍ فَجَعَلْتُم مِّنْهُ حَرَامًا وَحَلَالًا قُلْ آللَّـهُ أَذِنَ لَكُمْ ۖ أَمْ عَلَى اللَّـهِ تَفْتَرُونَ ﴿٥٩﴾

59. Sema: Je! Mwaonaje zile riziki alizo kuteremshieni Mwenyezi Mungu, nanyi mkafanya katika hizo nyengine haramu na nyengine halali. Sema:Je! Mwenyezi Mungu amekuruhusuni, au mnamzulia Mwenyezi Mungu tu?.

وَمَا ظَنُّ الَّذِينَ يَفْتَرُونَ عَلَى اللَّـهِ الْكَذِبَ يَوْمَ الْقِيَامَةِ ۗ إِنَّ اللَّـهَ لَذُو فَضْلٍ عَلَى النَّاسِ وَلَـٰكِنَّ أَكْثَرَهُمْ لَا يَشْكُرُونَ ﴿٦٠﴾

60. Na nini dhana ya wanaomzulia Mwenyezi Mungu kwa Siku ya Kiyama? Hakika Mwenyezi Mungu ana fadhila juu ya watu, lakini wengi wao hawashukuru.

Aya zilizotangulia zimezungumzia rehma na uongofu wa quran. Zikiendeleza yale yaliyokuja katika aya hizo aya hizi zinasema yule ambaye amejiweka mbali na quran hutumbukia kwenye mkumbo wa kufuata mambo ya uzushi na kubuni na kanuni zisizo na mashiko, ambayo yenyewe ni chanzo cha masaibu na matatizo mbali mbali yanayowatinga watu katika maisha yao. Kama ilivyo katika aya nyingine, quran tukufu inaashiria hapa tabia waliyokuwa nayo washirikina ya kujiharamishia kula wanyama wa miguu mine na baadhi ya mazao ya kilimo na badala yake wakivichukua vitu hivyo na kuviweka nadhiri kwa ajili ya masanamu yao.

Katika aya tulizosoma quran tukufu inawaambia washirikina hao kuwa riziki yenu nyinyi inatoka kwa Mwenyezi Mungu, na hivyo ni yeye ndiye mwenye haki ya kuamua kipi kiwe halali na kipi kiwe haramu kula, na wala

sio nyinyi; vinginevyo muonyeshe kama mumepata idhini kutoka kwake yeye Allah s.w.t ya kufanya hayo, hali ya kuwa nyinyi hamjapewa haki hiyo.

Hivyo basi mjiandae kwenda kujieleza siku ya Kiyama kuhusu uzushi na uwongo huo mliojitungia.

Aya zinaendelea kubainisha kuwa neema za Mwenyezi Mungu kwa waja ni kielelezo cha fadhila na ukarimu wake Mola lakini wanaadamu si washukurivu wa neema hizo ambazo huwaondokea kutokana na kuzusha kwao aina kwa aina za mambo ya upotofu na yasiyo na msingi.

Baadhi ya mambo tunayojifunza kutokana na aya hizi ni kuwa neema zote zinatoka kwa Mwenyezi Mungu na hivyo ni yeye ndiye mwenye haki ya kuhalalisha na kuharamisha vitu, na si wanadamu kutokana na utashi na matamanio yao ya kinafsi wajiamulie watakavyo kuhalalisha hiki na kuharamisha kile.

Aidha aya zinatutaka tuelewe kuwa aliye na mamlaka ya kuweka sheria kwa ajili ya wanadamu ni Allah pekee, na hivyo sheria yeyote inayotungwa na wanadamu ikakinzana na sheria yake ni bidaa na haina itibari.

### AYA YA 61

Aya ya 61 ndiyo inayotuhitimishia darsa yetu hii. Aya hiyo inasema:

وَمَا تَكُونُ فِي شَأْنٍ وَمَا تَتْلُو مِنْهُ مِن قُرْآنٍ وَلَا تَعْمَلُونَ مِنْ عَمَلٍ إِلَّا كُنَّا عَلَيْكُمْ شُهُودًا إِذْ
تُفِيضُونَ فِيهِ ۚ وَمَا يَعْزُبُ عَن رَّبِّكَ مِن مِّثْقَالِ ذَرَّةٍ فِي الْأَرْضِ وَلَا فِي السَّمَاءِ وَلَا أَصْغَرَ مِن ذَٰلِكَ
وَلَا أَكْبَرَ إِلَّا فِي كِتَابٍ مُّبِينٍ ﴿٦١﴾

61. Na huwi katika jambo lolote, wala husomi sehemu yoyote katika Quran, wala hamtendi kitendo chochote ila Sisi huwa ni mashahidi juu yenu mnapo shughulika nayo. Na hakifichikani kwa Mola wako Mlezi chenye uzito hata wa chembe katika ardhi na katika mbingu, wala kidogo kuliko hicho wala kikubwa ila kimo katika Kitabu kilicho wazi.

Aya hii inaashiria elimu isiyo na mpaka ya Allah s.w.t iliyo na utambuzi wa hali na harakati zote za mwanadamu, na kuelewa kila tendo litendwalo, liwe kubwa au dogo, la siri na la dhahiri, linalojiri kila mahala na katika kila sekunde, iwe ni katika ulimwengu wa mbinguni au wa ardhini na kuyahifadhi yote hayo katika lauhim mahfuudh.

Kwa hakika matendo yote ya waja, mbali na kushuhudiwa moja kwa moja na yeye Mola Karima yanaandikwa na kuhifadhiwa pia na malaika wake ambao huwa pamoja na waja ili kushuhudia na kuyanakili mazuri yote na mabaya yote wanayotenda.

Baadhi ya nukta za kuzingatiwa katika aya hii ni kuwa matendo yetu yote bali hata yale yanayotupitikia akilini na katika nafsi zetu yanashuhudiwa na kujulikana na Mwenyezi Mungu sw pamoja na malaika wake. Na kwa kweli hakuna chochote kinachofichika kwao.

Wapenzi wasomaji darsa yetu ya juma hili inaishia hapa. Tunamwomba Mola atulinde na hatari ya kuhalalisha vile alivyoviharamisha yeye na kuharamisha vile vilivyohalalishwa na yeye Mola Karima. Amin.

Wassalaamu Alaykum Warahmatullahi Wabarakaatuh.

5

# TAFSIRI YA SUURAT YUUNUS

## YUNUS 62-67

Bismillahir Rahmanir Rahim. Assalaamu Alaykum Warahmatullahi Wabarakaatuh.

Tunamshukuru Mwenyezi Mungu mtukufu kwa kutuwafikisha kukutana tena katika darsa yetu hii.

### ZA 62, 63 NA 64

Sura ya 10 ya Yunus ndiyo tunayoizungumzia kwa sasa, na hii ni darsa ya 318 tunayoianza kwa aya za 62, 63 na 64 ambazo zinasema:

أَلَا إِنَّ أَوْلِيَاءَ اللَّـهِ لَا خَوْفٌ عَلَيْهِمْ وَلَا هُمْ يَحْزَنُونَ ﴿٦٢﴾

62. Jueni kuwa vipenzi vya Mwenyezi Mungu hawatakuwa na khofu (siku ya Kiyama) wala hawatahuzunika.

الَّذِينَ آمَنُوا وَكَانُوا يَتَّقُونَ ﴿٦٣﴾

63. Nao ni wale ambao waliamini na wakawa wanamcha Mungu.

لَهُمُ الْبُشْرَىٰ فِي الْحَيَاةِ الدُّنْيَا وَفِي الْآخِرَةِ لَا تَبْدِيلَ لِكَلِمَاتِ اللَّـهِ ذَٰلِكَ هُوَ الْفَوْزُ الْعَظِيمُ ﴿٦٤﴾

64. Wao bishara njema katika maisha ya dunia na katika Akhera. Hapana mabadiliko katika maneno ya Mwenyezi Mungu. Huko ndiko kufuzu kukubwa.

Katika darsa kadhaa zilizopita tulisoma aya zilizozungumzia hali ngumu ya adhabu watakayokabiliana nayo wale waliokufuru na kumshirikisha Allah s.w.t Aya tulizosoma hivi punde zinabainisha hali watakayokuwa nayo waumini wa kweli waliomcha Mwenyezi Mungu, ili kwa kulinganisha hali za makundi mawili hayo iweze kufahamika ni ipi njia ya saada na ipi yenye mwisho mbaya.

Utulivu wa roho na kutopatwa na ghamu wala hali yoyote ya huzuni ni miongoni mwa neema kubwa ambazo Allah atawatunuku waja wake wema. Waja ambao kutokana na kujiweka mbali na madhambi na maovu waliweza kujikurubisha kwenye chemchemu ya usafi, mema na mazuri yote yaani Allah sw na kwa taabiri ya quran tukufu kuingia kwenye kundi la mawalii yaani vipenzi vya Mwenyezi Mungu.

Ni wazi kuwa nafsi za watu kama hao siku zote humiminikiwa na rehma za bishara njema za Mola Karima na hivyo katu huwa hawapatwi na shaka, ugoigoi au hali ya ulegevu katika kutekeleza majukumu yao ya kidini.

Bwana Mtume Muhammad **(s.a.w.w)** amesema: **"Kimya cha mawalii wa Mwenyezi Mungu ni dhikri, kutazama kwao ni ibra, maneno yao ni hikima na harakati zao katika jamii, ni sababu ya kupatikana baraka.**

Naye Imam Ali (a.s) amesema: **"Usije ukamdunisha mtu yoyote yule, kwani Mwenyezi Munguameficha mawalii wake miongoni mwa watu, hivyo si hasha yule umdunishaye akawa ni mmoja wao na wewe usijue"**.

Baadhi ya mafunzo tunayopata kutokana na aya hizi ni kuwa yule ambaye moyo wake unamkhofu Mwenyezi Mungu tu hawezi kumkhofu

yeyote mwengine. Aidha aya zinatuonyesha kuwa imani bila taqwa huwa haina athari; muumini wa kweli ni yule ambaye kila wakati anajichunga na kujiweka mbali na maovu na mambo machafu.

### AYA ZA 65 NA 66

Zifuatazo sasa ni aya za 65 na 66 za sura yetu ya Yunus ambazo zinasema:

وَلَا يَحْزُنكَ قَوْلُهُمْ إِنَّ الْعِزَّةَ لِلَّـهِ جَمِيعًا هُوَ السَّمِيعُ الْعَلِيمُ ﴿٦٥﴾

65. Wala yasikuhuzunishe maneno yao. Hakika utukufu wote ni wa Mwenyezi Mungu.Yeye ndiye asikiaye na ajuaye.

أَلَا إِنَّ لِلَّـهِ مَن فِي السَّمَاوَاتِ وَمَن فِي الْأَرْضِ وَمَا يَتَّبِعُ الَّذِينَ يَدْعُونَ مِن دُونِ اللَّـهِ شُرَكَاءَ إِن يَتَّبِعُونَ إِلَّا الظَّنَّ وَإِنْ هُمْ إِلَّا يَخْرُصُونَ ﴿٦٦﴾

66. Jueni kuwa ni vya Mwenyezi Mungu vyote vilivyomo mbinguni na ardhini. Na wala hawawafuati hao wanaowaomba badala ya Mwenyezi Mungu kuwa ni washirika wake. Wao hawafuati ila dhana tu na hawasemi ila uwongo.

Mushirikina wa Makka walikuwa wakimsingizia Bwana Mtume kila sifa mbovu kama vile kusema kwamba yeye ni mshairi, kuhani na mchawi bali hata mwendawazimu na wakisema: maneno haya ayasemayo Muhammad anafundishwa na watu wengine.

Na wakati mwingine wakisema kuwa yeye ni mtu kama wao tu wala lolote la ubora zaidi yao.

Katika kuyajibu maneno hayo yasiyo na msingi ya Mushirikina Allah sw anamliwaza Mtume wake kwa kumwambia, irada ya Mola wako imeshakata na kuhukumu kuwa wewe na wafuasi wako muwe na izza na utukufu; nao hao mushirikina hawawezi kufanya lolote kukabiliana na irada hiyo.

Na sababu ni kuwa ulimwengu na kila kilichomo ndani yake viko chini ya mamlaka yake Mola wako aliyetukuka, na kwa hivyo wale wanaowaendea waola ghairi ya Mwenyezi Mungu mtukufu si wao wenyewe wala hao waungu wao bandia walio na uwezo wa kufanya lolote.

Aya hii pamoja na mambo mengine inatuelimisha kuwa mojawapo ya mbinu zinazotumiwa na maadui wa Uislamu ni kuharibu haiba na shakhsiya ya viongozi wa dini hiyo tukufu.

Na hilo halikuishia katika zama za mwanzoni mwa kudhihiri kwa Uislamu bali linaendelea kushuhudiwa hata katika zama zetu hizi. Hata hivyo Allah sw ameshaahidi kuwa maadui hao katu hawatofanikiwa kwa kupitia njia hiyo kulifikia lengo lao hilo.

### AYA YA 67

Tunaihitimisha darsa yetu ya 318 kwa aya ya 67 ambayo inasema:

هُوَ الَّذِي جَعَلَ لَكُمُ اللَّيْلَ لِتَسْكُنُوا فِيهِ وَالنَّهَارَ مُبْصِرًا إِنَّ فِي ذَٰلِكَ لَآيَاتٍ لِّقَوْمٍ يَسْمَعُونَ ﴿٦٧﴾

67. Yeye (Mwenyezi Mungu) ndiye aliyekujaalieni usiku mpate kutulia humo, na mchana wa kuonea. Hakika katika hayo zimo ishara kwa watu wanaosikia.

Aya iliyopita imeashiria utawala mutlaki wa Allah s.w.t katika ulimwengu na kila kilichomo ndani yake.

Aya tuliyosoma ya 67 inagusia tadbiri yenye hikima kubwa ya Mola na kueleza kuwa mfumo wa mabadiliko ya usiku na mchana ni mojawapo ya madhihirisho ya uwezo wa Mola Mwenyezi katika uendeshaji wa ulimwengu.

Katika aya mbali mbali za quran usiku umetajwa kuwa kitoa utulivu cha mwanadamu. Ni wazi kwamba wakati ambapo utulivu wa kiwiliwili unayumkinika kwa kulala na kupumzika, utulivu wa roho hupatikana kwa dua, minong'ono na kushtakia mja hali yake kwa Mola na Muumba wake.

Aya hii pamoja na mambo mengine inatuelimisha kuwa mfumo tuushuhudiao wa ulimwengu haukutokea kwa bahati tu bali ni kitu kilichoumbwa na kuendeshwa kwa lengo na irada maalumu.

Kwa haya machache wapenzi wasomaji tunaifunga darsa yetu ya juma hili.

Inshallah Mwenyezi Mungu atujaalie kuwa miongoni mwa waja wake washukurivu wa neema zake na wanaozingatia na kuyatafakari maumbile ya ulimwengu ili kuweza kuitambua ipasavyo adhama ya Mola wao... Amin. Wassalamu Alaykum Warahmatullahi Wabarakaatuh.

## YUNUS 68-73

Assalaamu Alaykum Warahmatullahi Wabarakaatuh.

Karibuni katika mfululizo huu wa 319 wa darsa ya quran, tukiwa tunaendelea kuizungumzia sura ya 10 ya Yunus.

### AYA ZA 68, 69 NA 70

Tunaianza darsa yetu kwa aya za 68, 69 na 70 ambazo zinasema:

قَالُوا اتَّخَذَ اللَّـهُ وَلَدًا سُبْحَانَهُ هُوَ الْغَنِيُّ لَهُ مَا فِي السَّمَاوَاتِ وَمَا فِي الْأَرْضِ إِنْ عِندَكُم مِّن سُلْطَانٍ بِهَـٰذَا أَتَقُولُونَ عَلَى اللَّـهِ مَا لَا تَعْلَمُونَ ﴿٦٨﴾

68. Wamesema: Mwenyezi Mungu amejifanyia mtoto. Ameepukana na hayo. Yeye ni Mkwasi Mwenye kujitosheleza. Ni vyake vilivyomo mbinguni na vilivyomo ardhini. Nyinyi hamna uthibitisho wowote wa haya. Mnamzulia Mwenyezi Mungu msiyoyajua?

قُلْ إِنَّ الَّذِينَ يَفْتَرُونَ عَلَى اللَّـهِ الْكَذِبَ لَا يُفْلِحُونَ ﴿٦٩﴾

69. Sema: Wale wanaomzulia Mwenyezi Mungu uwongo hawatafaulu.

مَتَاعٌ فِي الدُّنْيَا ثُمَّ إِلَيْنَا مَرْجِعُهُمْ ثُمَّ نُذِيقُهُمُ الْعَذَابَ الشَّدِيدَ بِمَا كَانُوا يَكْفُرُونَ ﴿٧٠﴾

70. Hiyo ni starehe ya katika dunia tu, kisha kwetu ndiyo marejeo yao ni kwetu. Hapo tutawaonjesha adhabu kali kwa sababu ya kukufuru kwao.

Moja kati ya itikadi porofu na ya uzushi ambayo walikuwa nayo watu wa kaumu na uma zilizopita na ambayo inashuhudiwa pia hata hii leo ni kumjaalia Mwenyezi Mungu kuwa na wana na kuwanasibisha na yeye Mola Mwenyezi. Katika historia ya Uyahudi, wafuasi wa dini hiyo walimfanya Uzair mwana wa Mungu, nao wakristo wakatenda hayo hayo kuhusiana na Nabii Issa mwana wa Maryam. Hali ya kuwa kwanza kabisa ni kwamba Mwenyezi Mungu hana mke hata awe na mtoto.

**Pili**: ni kuwa Allah hahitaji kuwa na mwana, na tatu ni kwamba mtu ambaye ni kiumbe aliyeumbwa kamwe hawezi kuwa mwana wa Mungu

kwa sababu jinsia ya mtoto hutokana na ile ya wazazi wake wawili yaani baba na mama, hali ya kuwa kama tulivyotangulia kusema Mwenyezi Mungu aliyetukuka ametakasika na sifa ya kuwa na mke.

Kuhusiana na kauli zote hizo za batili na zisizo na mashiko quran tukufu inasema wale wanaotamka maneno hayo wajue kwamba lazima watawajibika kwayo, na siku ya kiyama watakuja kupata adhabu kali kwa sababu ya uzushi huo waliomnasbishia nao Mwenyezi Mungu (s.w.t)

Baadhi ya yale tunayojifunza kutokana na aya hizi ni kuwa Mola mtukufu hatishwi na upweke hata ahitajie mwana kwa ajili ya kuuondoa upweke huo.

Hahitajii msaada hata na awe na shida ya kuwa na msaidizi, na wala hachelei kuondoka hata iwepo haja ya mrithi wa baada yake. Subhanallah, ametakasika Mola aliyetukuka na kasoro zote hizo bali na nyinginezo.

Aidha aya zinatuonyesha kuwa lau mja angelinganisha mapungufu yaliyonayo maisha ya kupita ya dunia na hilaki ya adhabu isiyoweza kukadirika ya akhera basi angechunga na kujiweka mbali na kutamka mengi na kutenda mengi yanayomghadhibisha Mola wake.

### AYA YA 71

Ifuatayo sasa ni aya ya 71 ambayo inasema:

وَاتْلُ عَلَيْهِمْ نَبَأَ نُوحٍ إِذْ قَالَ لِقَوْمِهِ يَا قَوْمِ إِن كَانَ كَبُرَ عَلَيْكُم مَّقَامِي وَتَذْكِيرِي بِآيَاتِ اللَّـهِ فَعَلَى اللَّـهِ تَوَكَّلْتُ فَأَجْمِعُوا أَمْرَكُمْ وَشُرَكَاءَكُمْ ثُمَّ لَا يَكُنْ أَمْرُكُمْ عَلَيْكُمْ غُمَّةً ثُمَّ اقْضُوا إِلَيَّ وَلَا تُنظِرُونِ ﴿٧١﴾

71. Wasomee khabari za Nuhu alipowaambia watu wake: Enyi watu wangu! Ikiwa kukaa kwangu nanyi na kukumbusha kwangu Aya za Mwenyezi Mungu kunakuchukizeni, basi mimi namtegemea Mwenyezi Mungu. Nanyi tengenezeni mambo yenu na hao washirika wenu. Tena shauri lenu hilo lisifichikane kwenu. Kisha nihukumuni.Wala msinipe muhula.

Nabii Nuh (a.s) ni mmoja wa Mitume wateule wa Allah ambaye kwa miaka mingi sana alifanya kazi ya kuwalingania watu wa kaumu yake, lakini ni wachache tu miongoni mwao waliomuamini na akthari yao waliendelea kubaki kwenye shirki na ukafiri.

Aya hizi ambazo zilishuka huko Makka zinawaliwaza waislamu ambao walikuwa katika unyonge na hali ngumu ya maisha na kuwataka wawe na imani ya kupata msaada wa Mwenyezi Mungu na kuelewa kwamba Allah s.w.t yuko pamoja na wao na hivyo wasimame imara kama alivyosimama Nabii Nuh (a.s) ambaye licha ya vitisho na kila aina ya njama za wapinzani wa haki alisimama peke yake na kubeza nguvu na vitisho vyao kwa kuwaambia jumuikeni pamoja nyote na amueni chochote mnachotaka kuamua juu yangu, lakini jueni kwamba mimi nimetawakal kwa Mwenyezi Mungu na kutegemea nguvu na uwezo wake yeye tu.

Aya hii inatuelimisha kuwa historia ya waliotutangulia inabainisha wazi kwamba haki ni yenye kubaki na mwisho wa batili ni kutoweka na kwa hakika kuelewa yaliyojiri huko nyuma kunatoa mwanga wa kuonyesha njia ya huko tunakoelekea.

### AYA ZA 72 NA 73

Aya za 72 na 73 ndizo zinazotuhitimishia darsa yetu ya juma hili. Aya hizo zinasema:

فَإِن تَوَلَّيْتُمْ فَمَا سَأَلْتُكُم مِّنْ أَجْرٍ ۖ إِنْ أَجْرِيَ إِلَّا عَلَى اللَّـهِ ۖ وَأُمِرْتُ أَنْ أَكُونَ مِنَ الْمُسْلِمِينَ ﴿٧٢﴾

72. Lakini mkikengeuka (khiyari yenu). Mimi sikuombeni ujira. Ujira wangu hauko ila kwa Mwenyezi Mungu. Na nimeamrishwa niwe miongoni mwa wanaojisalimisha kwake.

فَكَذَّبُوهُ فَنَجَّيْنَاهُ وَمَن مَّعَهُ فِي الْفُلْكِ وَجَعَلْنَاهُمْ خَلَائِفَ وَأَغْرَقْنَا الَّذِينَ كَذَّبُوا بِآيَاتِنَا ۖ فَانظُرْ كَيْفَ كَانَ عَاقِبَةُ الْمُنذَرِينَ ﴿٧٣﴾

73. Lakini walimkadhibisha. Basi tukamuokoa pamoja na waliokuwa naye katika jahazi. Na tukawafanya wao ndio waliobakia. Na tukawazamisha wale waliozikadhibisha Aya zetu. Basi angalia vipi ulikuwa mwisho wa wale walioonywa (wasisikie).

Katika harakati yao ya kuwalingania watu njia ya Mwenyezi Mungu Mitume sio tu walikuwa tayari kukabiliana na hatari yoyote hata inayotishia maisha yao lakini pia hawakutarajia kupata chumo au mali yoyote ile ya dunia kwa sababu ya kazi hiyo nzito waliyokuwa wakifanya. Kwa maneno mengine ni kuwa hawakuwa wakitarajia chochote kwa watu mkabala wa kheri waliyokuwa wakiwafikishia.

Na ndiyo maana walikuwa wakiwaeleza bayana watu wao kwamba msidhani kuwa msipotuamini, kuna hasara tutakayopata kwani hatutarajii kupata ujira au malipo yoyote yale kutoka kwenu; sisi tunafanya yale tu tuliyoamrishwa na Mola wetu. Kisha aya zinaendelea kubainisha mwisho na hatima ya wapingaji haki na kueleza kuwa kwa kuteremka adhabu ya Mwenyezi Mungu na dhoruba kali, maji yalifunika kila kitu na ni wale waliokuwa wamepanda jahazi na Nabii Nuh ndio wao tu waliookoka na wakawa warithi wa ardhi, na kwamba hakuna mwisho mwingine unaowapata wale wanaoonywa wakapuuza zaidi ya huo uliowapata waliomkadhibisha Nauh as.

Kwa haya machache wapenzi wasomaji ndiyo tumefikia tamati ya darsa hii ya 319 ya quran. Tunamwomba Mwenyezi Mungu atulinde na kila aina ya shirki na kutuwafikisha kumwabudu kwa ikhlasi na kumtakasia dini yake. Amin.

Wassalaamu Alaykum Warahmatullahi Wabarakaatuh.

6

# TAFSIRI YA SUURAT YUUNUS

## YUNUS 74-78

Bismillahir Rahmanir Rahim. Assalaamu Alaykum Warahmatullahi Wabarakaatuh.

Tunamshukuru Mwenyezi Mungu mtukufu kwa kutuwafikisha kukutana tena katika darsa yetu hii.

### AYA 74 NA 75

Sura ya 10 ya Yunus ndiyo tunayoizungumzia kwa sasa, na hii ni darsa ya 320 tunayoianza kwa aya 74 na 75 ambazo zinasema:

ثُمَّ بَعَثْنَا مِن بَعْدِهِ رُسُلًا إِلَىٰ قَوْمِهِمْ فَجَاءُوهُم بِالْبَيِّنَاتِ فَمَا كَانُوا لِيُؤْمِنُوا بِمَا كَذَّبُوا بِهِ مِن قَبْلُ كَذَٰلِكَ نَطْبَعُ عَلَىٰ قُلُوبِ الْمُعْتَدِينَ ﴿٧٤﴾

74. Kisha tukawapeleka Mitume (wengi) baada yake kwa watu wao. Nao wakawajia na hoja waziwazi. Lakini hawakuwa wenye kuamini waliyoyakadhibisha kabla yake.

ثُمَّ بَعَثْنَا مِن بَعْدِهِم مُّوسَىٰ وَهَارُونَ إِلَىٰ فِرْعَوْنَ وَمَلَئِهِ بِآيَاتِنَا فَاسْتَكْبَرُوا وَكَانُوا قَوْمًا مُّجْرِمِينَ ﴿٧٥﴾

75. Namna hivi tunapiga muhuri juu ya nyoyo za watu warukao mipaka." Kisha baada ya hao tukamtuma Musa na Haruni kwa Firauni na watu wake wakubwa, kwa hoja zetu. Lakini walijivuna, wakawa watu maasi.

Aya tulizosoma zinaashiria utaratibu alioweka Mwenyezi Mungu mtukufu kuhusiana na utumaji wa Mitume mmoja baada ya mwingine kwa ajili ya kuwafikishia waja wake risala ya uongofu na kusema kuwa manabii walikuwa na miujiza mbali mbali kwa ajili ya kuthibitisha ukweli kwamba risala walizokuja nazo zinatoka kwa Mwenyezi Mungu mtukufu.

Na kwa hakika ukweli huo uliwathibitikia wale waliofikishiwa risala hizo. Pamoja na hayo akthari ya watu hawakuwa tayari kuikubali haki kutokana na kutopea kwenye ufuska na mambo machafu vitu ambavyo havikubaliani na sifa ya kushikamana na mafundisho ya dini.

Ijapokuwa wakati ilipotokea tufani ya gharika katika enzi za Nabii Nuh (a.s) makafiri wote waliangamizwa, na ni wale tu waliokuwa wamemwamini Mtume huyo na kuabiri pamoja naye jahazini ndio waliookoka, lakini baada ya Nabii huyo walizuka tena makafiri na mushirikina wengi na hivyo na kupelekea Mwenyezi Mungu kutuma manabii wengine kadhaa wakiwemo Ibrahim, Ismali, Hud, Saleh, Yaaqub, Yusuf n.k.

Pamoja na hayo watu waliendelea kuonyesha inadi, ukaidi na upinzani dhidi ya haki na kama walivyokuwa wakanushaji waliowatangulia hawakuwa tayari kuacha maovu ya kiitikadi na kimatendo na kuamini wito wa haki.

Baada ya manabii hao, Nabii mwingine mteule yaani Musa as akiwa pamoja na ndugu yake Harun amani ya Allah iwe juu yake, walitumwa kwa Firauni ili kumfikishia wito wa Lailaha illa llah. Lakini naye pia pamoja na watu wake walitakabari na kuipa mgongo haki.

Baadhi ya mafunzo tunayoyapata kutokana na aya hizi ni kuwa Allah sw amehakikisha kwamba anawapelekea waja wake Mitume wa kuwalingania uongofu, lakini wakati huo huo amempa mwanadamu uhuru kamili wa kuchagua kati ya kuamini na kuikufuru haki, kwani hakutaka mwanadamu aiamini na kuifuata dini yake ya haki kwa kulazimishwa na kutezwa nguvu.

### AYA ZA 76 NA 77

Zifuatazo sasa ni aya za 76 na 77 ambazo zinasema:

فَلَمَّا جَاءَهُمُ الْحَقُّ مِنْ عِندِنَا قَالُوا إِنَّ هَـٰذَا لَسِحْرٌ مُّبِينٌ ﴿٧٦﴾

76. Basi ilipowajia haki kutoka kwetu walisema: Bila shaka huu ni uchawi dhahiri.

قَالَ مُوسَىٰ أَتَقُولُونَ لِلْحَقِّ لَمَّا جَاءَكُمْ ۖ أَسِحْرٌ هَـٰذَا وَلَا يُفْلِحُ السَّاحِرُونَ ﴿٧٧﴾

77. Akasema Musa: Mnasema (hivi) juu ya haki ilipokujieni? Huu ni uchawi? Na wachawi hawafaulu!.

Mojawapo ya mbinu zilizokuwa zikitumiwa na wapinzani wa Mitume na hasa wale vigogo wa ukafiri na shirki ilikuwa ni kuzusha tuhuma zisizo na msingi kwa waja hao wateule wa Allah.

Na ndiyo maana Quran tukufu inaeleza kuwa takriban Mitume wote hawakusalimika na tuhuma za kusingiziwa kuwa ni wachawi, ili miujiza waliyokuja nayo ionekane kuwa ni vitendo vya hila na hadaa na wao wenyewe wachukuliwe kuwa ni watu wajanja na matapeli. Kama aya zinavyoeleza, wakati Firauni alipoona ameshindwa kukabiliana na hoja za kimantiki za wito wa haki wa Nabii Musa aliamuru wachawi wake wote wakusanywe pamoja ili kumfanya Mtume huyo wa Allah aonekane naye pia kuwa ni mchawi tu kama walivyo wachawi wake.

Hali ya kuwa alichokuwa akikieleza Nabii Musa ni kwamba nyinyi kina Firauni na watu wenu hamjawahi kunishuhudia hapo kabla nikifanya uchawi au kiini macho, lakini sasa nimekuja na wito wa haki na kuthibitisha ukweli wa Utume wangu kwa kukuonyesheni muujiza mnanisingizia kuwa ni mchawi na maneno yangu nayo mnadai kuwa ni uchawi. Ukweli ni kuwa hicho ni kisingizio tu kwa ajili ya kuipa mgongo haki.

Baadhi ya mafunzo tunayopata kutokana na aya hizi ni kuwa viongozi wa dini wanatakiwa waelewe kuwa siku zote watakuwepo watu katika jamii watakaowapiga vita na kuipinga haki na hata kutaka haki hiyo ionekane kuwa ni batili.

### AYA YA 78

Wapenzi wasomaji, darsa ya 320 inahitimishwa na aya ya 78 ambayo inasema:

قَالُوا أَجِئْتَنَا لِتَلْفِتَنَا عَمَّا وَجَدْنَا عَلَيْهِ آبَاءَنَا وَتَكُونَ لَكُمَا الْكِبْرِيَاءُ فِي الْأَرْضِ وَمَا نَحْنُ لَكُمَا بِمُؤْمِنِينَ ﴿٧٨﴾

78. Wakasema: Je umetujia ili utuachishe tuliyowakuta nayo baba zetu na ili ukubwa uwe wenu nyinyi (wawili) katika nchi (hii)? Wala sisi hatukuaminini nyinyi.

Kwa sababu ya kuonyesha heshima ya wazee wao waliowatangulia watu wengi huwa hawako tayari kuacha mila na desturi walizozioea na kurithi kutoka kwao, na kujenga dhana kwamba kila kilichosemwa na hao mababa

na mababu zao kilikuwa sahihi, na mtu yeyote yule hana haki ya kusema kinyume na dhidi ya hayo. Hali ya kuwa kuwaheshimu waliotangulia ni kitu kimoja na kung'ang'ania bila hoja bali kwa taasubi na ukereketwa tu kila lililosemwa na kutendwa na wao, na kuhisi sisi wa baada ya wao tufanye kile kile kilichofanywa na wao hata kama si sahihi, hicho nacho ni kitu kingine kabisa.

Na ni kwa mantiki hiyo isiyo sahihi, ndio maana wapinzani wa Mitume walikuwa wakishikilia kwamba maadamu wazee wetu walikuwa wakiabudu masanamu, sisi hatuko tayari kuamini bali hata kusikia kitu kingine ghairi ya hicho. Funzo mojawapo tunalopata kutokana na aya hii ni kuwa kushikilia kufuata kibubusa itikadi potofu za waliotangulia ni miongoni mwa sababu kuu zilizowafanya watu wengi wapinge risala za Mitume wao. Wapenzi wasomaji darsa ya 320 imefikia tamati. Tunamwomba Allah atuonyeshe haki na kutuwafikisha kuifuata, na atuonyeshe batili na kutuwezesha kuiepuka. Amin.

Wassalaamu Alaykum Warahmatullahi Wabarakaatuh.

7

# TAFSIRI YA SUURAT YUUNUS

## YUNUS 79-86

Bismillahir Rahmanir Rahim. Assalaamu Alaykum Warahmatullahi Wabarakaatuh.

Karibuni katika mfululizo mwingine wa darsa ya quran.

### AYA ZA 79 NA 80

Hii ni darsa ya 321, na tukiwa tunaendelea kuizungumzia sura ya 10 ya Yunus tunaianza darsa yetu kwa aya za 79 na 80 ambazo zinasema:

وَقَالَ فِرْعَوْنُ ائْتُونِي بِكُلِّ سَاحِرٍ عَلِيمٍ ﴿٧٩﴾

79. Na akasema Firauni: Nileteeni kila mchawi mjuzi.

فَلَمَّا جَاءَ السَّحَرَةُ قَالَ لَهُم مُّوسَىٰ أَلْقُوا مَا أَنتُم مُّلْقُونَ ﴿٨٠﴾

80. Basi walipokuja wachawi, Musa aliwaambia: Tupeni mnavyotaka kuvitupa.

Katika darsa iliyopita tulisema kuwa Nabii Musa as alitakiwa na Mola wake aianze kazi yake ya kulingania La ilaha illa llah kwa kumwendea Firauni na kumtaka aikubali tauhidi yaani kumuabudu Mungu mmoja wa haki na pia kuwakomboa Bani Israil na madhila ya Mafirauni.

Aya tulizosoma zinasema Firauni, ambaye hakuwa na uwezo wa kukabiliana na huja na burhani alizopewa na Musa (a.s) alianza kuutuhumu muujiza alioonyeshwa na Nabii huyo kuwa ni uchawi na hivyo kutoa amri ya kuitwa wachawi wake wote ili kukabiliana na muujiza huo wa Mtume wa Allah Musa (a.s).

Lakini Nabii Musa ambaye hakuwa na chembe ya shaka kuwa haki iko upande wake aliwataka wachawi wa Firauni wafanye kila walichonacho cha uchawi na mazingaombwe yao ili watu wajionee wenyewe na kuamua. Hivyo miongoni mwa yale tunayojifunza kutokana na aya hizi ni kuwa mataghuti wa kila zama huamua kuwatumia vibaya wataalamu na taaluma zao ili kuweza kufikia malengo yao maovu.

Aidha aya hizi zinatuelimisha kuwa Mitume walikuwa na yakini na risala waliyokuwa wakiilingania, na juu ya kupata nusra na msaada wa Allah sw.

### AYA ZA 81 NA 82

Tunaiendeleza darsa yetu hii kwa aya za 81 na 82 ambazo zinasema:

فَلَمَّا أَلْقَوْا قَالَ مُوسَىٰ مَا جِئْتُم بِهِ السِّحْرُ ۖ إِنَّ اللَّـهَ سَيُبْطِلُهُ ۖ إِنَّ اللَّـهَ لَا يُصْلِحُ عَمَلَ الْمُفْسِدِينَ ﴿٨١﴾

81. Walipotupa, Musa alisema: Mliyoleta ni uchawi; Mwenyezi Mungu sasa hivi ataubatilisha. Hakika Mwenyezi Mungu haitengenezi kazi ya waharibifu.

وَيُحِقُّ اللَّـهُ الْحَقَّ بِكَلِمَاتِهِ وَلَوْ كَرِهَ الْمُجْرِمُونَ ﴿٨٢﴾

82. Na Mwenyezi Mungu ataithubutisha haki kwa maneno yake, ingawa watachukia hao wabaya.

Kama ilivyoelezwa pia katika suratu Shuaraa, wachawi wa Firauni walitupa kamba zao na vifimbo vyao, na kutamka kuwa kwa utukufu wa

Firauni tunaapa kuwa sisi ndio washindi. Hakika ni kuwa wachawi wa Firauni hawakufanya chochote kubadilisha kamba na vifimbo vyao, bali walifanya kiini macho tu na hivyo watu wakahisi kana kwamba vifimbo na kamba hizo zilikuwa zinaonyesha harakati za kutambaa.

Na ndiyo maana Nabii Musa aliwatangazia kinagaubaga kuwa Mwenyezi Mungu atauanika hadharani ubatili wa uchawi wao huo na kuithibitisha haki mbele ya macho ya watu.

Baadhi ya nukta za kuzingatiwa katika aya hizi ni kuwa hata kama batili itarembwa na kupambwa kwa kila namna ya urembo mwishowe itabainika na kutoweka tu.

Nukta nyingine ya kuzingatiwa katika aya hizi ni kuwa nia na njama ya mustakbirina ya kutaka kuizima nuru ya haki haiwezi kufaulu na kusimama mbele ya irada ya Allah s.w.t ambaye ameahidi kuwa nusra na msaada wake hautoacha kuwafikia wale waliosimama upande wa haki.

### AYA YA 83

Tunaiendeleza darsa yetu kwa aya ya 83 ambayo inasema:

فَمَا آمَنَ لِمُوسَىٰ إِلَّا ذُرِّيَّةٌ مِّن قَوْمِهِ عَلَىٰ خَوْفٍ مِّن فِرْعَوْنَ وَمَلَئِهِمْ أَن يَفْتِنَهُمْ ۚ وَإِنَّ فِرْعَوْنَ لَعَالٍ فِي الْأَرْضِ وَإِنَّهُ لَمِنَ الْمُسْرِفِينَ ﴿٨٣﴾

83. Hawakumuamini Musa isipokuwa baadhi ya vijana wa kaumu yake kwa kumuogopa Firauni na wakuu wao, wasiwatese. Kwani hakika Firauni alikuwa jeuri katika nchi. Na kwa yakini alikuwa miongoni mwa (maasi) waliopita mpaka.

Katika awamu ya kwanza ya kazi yake ya kulingania laa ilaha illa llah, Nabii Musa [a.s] alimwendea Firauni na wasaidizi wake kisha katika awamu ya pili akakabiliana na wachawi na kuwashinda .

Ama katika hatua ya tatu aliwafuata watu wa Bani Israil ambapo mwanzo wake ni vijana wa kaumu hiyo ndio waliomuamini.

Tabaan vijana hao nao waliamini pamoja na kwamba walikuwa wakikabiliwa na mateso na madhila ya Firauni.

Miongoni mwa yale tunayojifunza na kutokana na aya hii ni kuwa tabaka la kwanza kumwamini Musa katika Bani Israil lilikuwa ni tabaka la vijana, na hii ni kwa sababu nyoyo ya za vijana huwa safi na bongo zao huwa pia hazijakomazwa na fikra za kitaasubi. Halikadhalika aya hii inatuonyesha kuwa hata katika mifumo inayotawaliwa na mafirauni, mtu anaweza kujivua na upotofu wa mfumo huo na kushikamana na njia ya haki ya akina Musa [a.s].

### AYA ZA 84, 85 NA 86

Darsa ya 231 inahitimishwa na aya za 84, 85 na 86 ambazo zinasema:

وَقَالَ مُوسَىٰ يَا قَوْمِ إِن كُنتُمْ آمَنتُم بِاللَّهِ فَعَلَيْهِ تَوَكَّلُوا إِن كُنتُم مُّسْلِمِينَ ﴿٨٤﴾

84. Na Musa akasema: "Enyi kaumu yangu Ikiwa nyinyi mumemwamini Mwenyezi Mungu, basi mtegemeeni yeye kama nyinyi ni Waislamu kweli.

فَقَالُوا عَلَى اللَّهِ تَوَكَّلْنَا رَبَّنَا لَا تَجْعَلْنَا فِتْنَةً لِّلْقَوْمِ الظَّالِمِينَ ﴿٨٥﴾

85. Wakasema: Tunamtegemea Mwenyezi Mungu. Ee Mola wetu. Usitufanye wenye kutiwa misukosuko na hao watu madhalimu.

وَنَجِّنَا بِرَحْمَتِكَ مِنَ الْقَوْمِ الْكَافِرِينَ ﴿٨٦﴾

86. Na utuokoe kwa rehama yako na hao watu makafiri.

Katika kukabiliana na mateso makali na maudhi na madhila ya akina Firauni, Nabii Musa (a.s) aliwataka watu wa kaumu yake watawakal kwa Mwenyezi Mungu na kuwaonyesha kuwa kutawakkal na kumtegemea Allah tu na kusalimisha muislamu mambo yake yote kwa Mola wa haki ni sharti la imani ya kweli. Nao wale waliokuwa wamemuamini kikweli kweli Musa as waliyasikiliza mawaidha hayo waliyopewa na Mtume wao na kusema, sisi hatuna kimbilio wala egemeo jengine ghairi ya Allah sw na hivyo tunamuelekea yeye na kumwomba atulinde na shari ya madhalimu na makafiri.

Baadhi ya mafunzo tunayoyapata kutokana na aya hizi ni kuwa wakati wa masaibu na misukosuko Mola Mwenyezi huwa ndiye tegemeo pekee la mja muumini, na kwa kweli kwa kumtegemea yeye Mola aliye Muweza wa kila kitu na kujisalimisha kwake kwa kushikamana na maamrisho yake na kujiepusha makatazo yake, mja huweza kufaulu katika kukabiliana na misukosuko yoyote inayomkuta.

Aidha kutokana na aya hii tunajielimisha kuwa dua na kushtakia hali yake mja kwa Mola, ni miongoni mwa njia za kumnasua mja na mazonge. Kwa haya machache tunaifunga darsa yetu ya juma hili na kumwomba Mola aijaze subra ndani ya nyoyo zetu, athibitshe imani zetu na atunusuru na kila fitna inayoweza kutuweka mbali na dini yetu. Amin.

Wassalaamu Alaykum Warahmatullahi Wabarakaatuh.

## YUNUS 87-92

Assalaamu Alaykum Warahmatullahi Wabarakaatuh. Karibuni katika mfululizo mwingine wa darsa ya quran.

## AYA YA 87

Hii ni darsa ya 322, na tukiwa tunaendelea kuizungumzia sura ya 10 ya Yunus, tunaianza darsa yetu kwa aya ya 87 ambayo inasema:

وَأَوْحَيْنَا إِلَىٰ مُوسَىٰ وَأَخِيهِ أَن تَبَوَّآ لِقَوْمِكُمَا بِمِصْرَ بُيُوتًا وَاجْعَلُوا بُيُوتَكُمْ قِبْلَةً وَأَقِيمُوا الصَّلَاةَ ۗ وَبَشِّرِ الْمُؤْمِنِينَ ﴿٨٧﴾

87. Na tukampelekea Musa na ndugu yake wahyi ya kwamba: Watengenezeeni majumba watu wenu katika Misri na zifanyeni nyumba zenu zielekeane, na mshike Sala na wabashirie Waumini.

Ili kuijenga tena jamii ya Bani Israil, baada ya kuikomboa na madhila ya Firaun, Nabii Musa (a.s) aliamriwa na Mola wake kuwakusanya watu wa kaumu yake mahali pamoja na kwa msaada wao kujenga nyumba kwa ajili ya makaazi yao.

Nyumba hizo zilitakiwa ziweko mahali pamoja zikiwa zimeelekeana na si kutawanyika huku na huko ili iwe rahisi kwao kujumuika pamoja kwa ajili ya kupanga na kuchukua maamuzi mbali mbali ya kijamii, na pia endapo Firauni atataka kuwaangamiza waweze kusimama pamoja na kukabiliana naye.

Baadhi ya wafasiri wa quran wanasema, kutokana na kutolewa amri ya sala katika aya hii, muradi uliokusudiwa hapa juu ya neno qibla ni kuzijenga

nyumba zao hizo kwa namna ambayo zitakuwa zimeelekea upande wa kibla ili wakiwa ndani ya nyumba zao waweze kutekeleza ibada zao. Pamoja na hayo maana hiyo ni ya kiistilahi, na kimsingi makusudio ya neno qibla kilugha ni maana hiyo hiyo ya kuelekeana.

Baadhi ya mafunzo tunayopata kutokana na aya hizi ni kuwa mojawapo ya sifa za Mitume ilikuwa ni kuwafikiria watu na hivyo kila wakati wakichukua hatua zinazohitajika kwa ajili ya kuwasaidia watu wa kaumu zao.

Funzo jengine tunalopata kutokana na aya hii ni kuwa kushughulika na masuala ya kimaada na kimaisha kusitughafilishe na utekelezaji wa sala na kumwabudu Mola wetu. Kutekeleza kwa pamoja yote hayo ndiko kutakakotufanya tupate rehma na baraka za Mola Karima.

### AYA ZA 88 NA 89

Zifuatazo sasa ni aya za 88 na 89 ambazo zinasema:

وَقَالَ مُوسَىٰ رَبَّنَا إِنَّكَ آتَيْتَ فِرْعَوْنَ وَمَلَأَهُ زِينَةً وَأَمْوَالًا فِي الْحَيَاةِ الدُّنْيَا رَبَّنَا لِيُضِلُّوا عَن سَبِيلِكَ رَبَّنَا اطْمِسْ عَلَىٰ أَمْوَالِهِمْ وَاشْدُدْ عَلَىٰ قُلُوبِهِمْ فَلَا يُؤْمِنُوا حَتَّىٰ يَرَوُا الْعَذَابَ الْأَلِيمَ ﴿٨٨﴾

88. Na Musa akasema: Mola wetu! Hakika wewe umempa Firauni na watu wake wakubwa mapambo na mali katika maisha ya dunia. Mola wetu! Hivyo wanapoteza watu na Njia yako. Mola wetu! Ziangamize mali zao na zifunge nyoyo zao, wasiamini mpaka waione adhabu chungu.

قَالَ قَدْ أُجِيبَت دَّعْوَتُكُمَا فَاسْتَقِيمَا وَلَا تَتَّبِعَانِّ سَبِيلَ الَّذِينَ لَا يَعْلَمُونَ ﴿٨٩﴾

89. Mwenyezi Mungu akasema: Maombi yenu yamekubaliwa. Basi simameni sawasawa, wala msifuate njia za wale wasiojua.

Katika kuendelea na utekelezaji wa jukumu alilopewa na Mola wake la kupambana na Firaun, Nabii Musa (a.s) alimwomba Allah s.w.t auangamize utajiri uliopindukia mpaka aliokuwa nao Firaun na kutomruhusu aendelee kufanya ufisadi na uharibifu, pamoja na kutumia vibaya nguvu na mamlaka aliyokuwa nayo kutokana na utajiri na neema za kimaada alizoruzukiwa na yeye Mola Karima; mali na neema ambazo alikuwa akizitumia kwa ajili ya kupotosha watu na njia ya Mwenyezi Mungu.

Nabii Musa aliomba dua hiyo kwa Mwenyezi Mungu pale ilipofika hadi akawa hana matumaini tena kwamba Firauni ataamini na kuikubali haki.

Allah s.w.t aliitakabalia dua ya Mtume wake, na hivyo akamtaka Mussa as na watu wake wao wenyewe kwanza wasimame sawa sawa na kushikamana na njia ya Mola wao; kwani sharti mojawapo la kutakabaliwa dua ni waumini wenyewe kwanza kuwa wameshikamana barabara na njia ya uongofu. Na ndiyo maana kwa mujibu wa hadithi ni kwamba ilichukua muda wa miaka arubaini tokea Nabii Musa alipoomba dua ya kumwapiza Firauni hadi taghuti huyo alipoangamizwa kwa kugharikishwa baharini.

Aya hizi pamoja na mambo mengine zinatufunza kwamba, kuwa na utajiri wa mali tu si kipimo cha kuonyesha kuwa Mwenyezi Mungu amemjali na kumpenda mja. Kwani katika dunia hii, hata makafiri nao wamepewa neema nyingi za kimaada.

Halikadhalika aya zinatuonyesha kuwa pamoja na sisi kumwomba Mola awaangamize madhalimu, sisi wenyewe pia tujihimu na kutekeleza wajibu wetu ipasavyo.

### AYA ZA 90, 91 NA 92

Darsa ya 322 inahitimishwa na aya za 90, 91 na 92 ambazo zinasema:

وَجَاوَزْنَا بِبَنِي إِسْرَائِيلَ الْبَحْرَ فَأَتْبَعَهُمْ فِرْعَوْنُ وَجُنُودُهُ بَغْيًا وَعَدْوًا ۖ حَتَّىٰ إِذَا أَدْرَكَهُ الْغَرَقُ قَالَ آمَنتُ أَنَّهُ لَا إِلَٰهَ إِلَّا الَّذِي آمَنَتْ بِهِ بَنُو إِسْرَائِيلَ وَأَنَا مِنَ الْمُسْلِمِينَ ﴿٩٠﴾

90. Tukawavusha bahari wana wa Israili, na Firauni na askari wake wakawafuata kwa dhulma na uadui. Hata Firauni alipokuwa anataka kuzama akasema: "Naamini kuwa hapana mungu ila yule waliyemuamini Wana wa Israili, na mimi ni miongoni mwa wanaonyenyekea.

آلْآنَ وَقَدْ عَصَيْتَ قَبْلُ وَكُنتَ مِنَ الْمُفْسِدِينَ ﴿٩١﴾

91. Ala! Sasa (unaamini hayo)? Na hali uliasi kabla yake na ukawa miongoni mwa mafisadi!.

فَالْيَوْمَ نُنَجِّيكَ بِبَدَنِكَ لِتَكُونَ لِمَنْ خَلْفَكَ آيَةً ۚ وَإِنَّ كَثِيرًا مِّنَ النَّاسِ عَنْ آيَاتِنَا لَغَافِلُونَ ﴿٩٢﴾

92. Leo basi tutakuokoa kwa kuuweka mwili wako, ili uwe ishara kwa ajili ya walio nyuma yako. Na hakika watu wengi wameghafilika na ishara zetu.

Aya hizi wapenzi wasomaji zinabainisha jinsi dua iliyoombwa na Nabii Musa as ilivyotakabaliwa, na kueleza kuwa pale jeshi la Firauni lilipoamua kukuandameni nyinyi kwa lengo la kukuangamizeni, sisi tulikufungulieni njia katika mto Nile na kukupitisheni salama usalimini. Ama Firauni na jeshi lake wao tuliwagharikisha kwenye mto huo na tukaamua kukiibua kutoka majini kiwiliwili cha Firauni tu peke yake, ili hilo liwe funzo na ibra kwa wengine.

Nukta yenye kutoa mguso hapa ni kuwa ule utabiri wa Nabii Musa tuliouona katika aya iliyotangulia ulithibiti na kuwa kweli, kwani wakati Firauni alipoiona adhabu ya kugharikishwa imemkabili hapo alitamka kwa unyenyekevu kuwa amemwamini Mola wa haki waliyemuamini Bani Israil.

Lakini wapi! jibu alilopata ni kuwa, hivi sasa wakati mauti yamekukabili ndiyo unatubia na kuiamini haki.

Hayo ni majuto matupu yaliyopitwa na wakati na majuto ni mjukuu. Miongoni mwa yale tunayojifunza kutokana na aya hizi ni kuwa katika kupambana na mataghuti, tutawakal na kumtegemea Mwenyezi Mungu tu, kwani yeye hatotuacha mkono bali atatufungulia njia ya faraja hata pale tutakapkuwa katika hali ngumu kabisa ya misukosuko.

Funzo jengine tunalopata hapa ni kuwa, kama sisi tutasimama imara na bila kutetereka katika njia ya laa ilaha illa llah mataghuti hawatokuwa na jengine la kufanya ghairi ya kupiga magoti na kusalimu amri, na kupata jaza ya maovu yao.

Aidha aya zinatuonyesha kuwa kuna umuhimu wa kuzitunza na kuzihifadhi athari na turathi za watu waliotangulia zinazoonyesha uwezo wa Allah sw, ili ziwe funzo na mazingatio kwetu sisi na watakaokuja baada yetu. Kwa haya machache tunaifunga darsa yetu hii, kwa kumwomba Allah atuwafikishe kutubia makosa yetu mara tu tunapoteleza, na kupata maghufira na msamaha wake kabla ya kufikwa na mauti. Amin.

Wassalaamu Alaykum Warahmallahi Wabarakaatuh.

8

# TAFSIRI YA SUURAT YUUNUS

## YUNUS 93-97

Bismillahir Rahmanir Rahim. Alaykum Warahmatullahi Wabarakaatuh. Karibuni katika mfululizo huu wa 323 wa darsa ya quran, tukiwa tunaendelea kuizungumzia sura ya 10 ya Yunus.

### AYA YA 93

Tunaianza darsa yetu kwa aya ya 93 ambayo inasema:

وَلَقَدْ بَوَّأْنَا بَنِي إِسْرَائِيلَ مُبَوَّأَ صِدْقٍ وَرَزَقْنَاهُم مِّنَ الطَّيِّبَاتِ فَمَا اخْتَلَفُوا حَتَّىٰ جَاءَهُمُ الْعِلْمُ إِنَّ رَبَّكَ يَقْضِي بَيْنَهُمْ يَوْمَ الْقِيَامَةِ فِيمَا كَانُوا فِيهِ يَخْتَلِفُونَ ﴿٩٣﴾

93. Na hakika tuliwaweka Wana wa Israili makazi mazuri, na tukawaruzuku vitu vizuri. Nao hawakukhitalifiana mpaka ilipowafikia ilimu. Hakika Mola wako atahukumu baina yao Siku ya Kiyama katika yale waliyokuwa wakikhitalifiana.

Katika aya hii Mwenyezi Mungu s.w.t ameashiria neema kadha wa kadha alizowapa Bani Israil na kusema kuwa baada ya miaka na miaka ya kutangatanga na kutokuwa na pa kukaa tuliwapa Bani Israil eneo lenye hali nzuri kabisa ya hewa, na lenye rutuba na ustawi huko Sham na kuwaruzuku riziki zilizo bora kabisa.

Lakini badala ya kushukuru kwa hayo na kuwa watiifu wa kushikamana na maamrisho tuliyowateremshia wakaanza kufarikiana na kutengana na kila mmoja akaamua kufuata njia yake. Hivyo kila mmoja atatakiwa kuja kuutolea maelezo mwenendo huo muovu aliokuwa nao atakaposimamishwa mbele ya mahakama ya uadilifu siku ya Kiyama.

Baadhi ya mafunzo tunayopata kutokana na aya hii ni kuwa katika mafundisho ya Mitume, mbali na kuzingatiwa suala la kuwalea na kuwajenga watu kiroho na kimaanawi, yanazingatiwa vile vile mahitaji yao ya kimaada kwa kuwapa uhuru, fursa na suhula za kimaisha za kupatia riziki safi na za halali.

Aidha aya hii inatuonyesha kuwa hitilafu na mifarakano hutokana na kujiweka mbali watu na mafundisho ya mbinguni na hilo huwa sababu ya kuondokewa na neema za Mola wao.

### AYA ZA 94 NA 95

Tunaiendeleza darsa yetu kwa aya za 94 na 95 ambazo zinasema:

فَإِن كُنتَ فِي شَكٍّ مِّمَّا أَنزَلْنَا إِلَيْكَ فَاسْأَلِ الَّذِينَ يَقْرَءُونَ الْكِتَابَ مِن قَبْلِكَ لَقَدْ جَاءَكَ الْحَقُّ مِن رَّبِّكَ فَلَا تَكُونَنَّ مِنَ الْمُمْتَرِينَ ﴿٩٤﴾

94. Na kama unayo shaka juu ya hayo tuliyokuteremshia, basi waulize wasomao kitabu kabla yako. Kwa yakini imekwisha kujia haki kutoka kwa Mola wako. Basi usiwe miongoni mwa wenye shaka.

وَلَا تَكُونَنَّ مِنَ الَّذِينَ كَذَّبُوا بِآيَاتِ اللَّـهِ فَتَكُونَ مِنَ الْخَاسِرِينَ ﴿٩٥﴾

95. Na kabisa usiwe miongoni mwa wale wanaozikanusha ishara za Mwenyezi Mungu usije ukawa miongoni mwa wenye khasara.

Aya hizi wapenzi wasomaji zinawahutubu wale waliokuwa na shaka kama yale aliyokuja nayo Bwana Mtume Muhammad **(s.a.w.w)** ni maneno ya haki au la na kuwaambia kwamba ikiwa mtavirejea vitabu vya mbinguni vilivyotangulia mtaona humo bishara na alama za Mtume Muhammad **(s.a.w.w)** Mbali na hayo mtashuhudia pia kuwa zimezungumzwa na vitabu hivyo hatima za kaumu nyingi zilizotangulia zilizotajwa pia ndani ya Quran kama vile bani Israil, na hivyo kukubainikieni kwamba hii Quran pia ni kitabu cha haki kinachotoka kwa Mwenyezi Mungu s.w.t

Ni wazi kuwa kama shaka yenu itaondolewa baada ya kubaini hayo na kutambua kuwa Quran ni kitabu cha haki, kukadhibisha kwenu kitabu hicho baada ya kubainikiwa na hayo kutakuwa ni kwa madhara yenu yenyewe kutokana na kujinyima fursa ya kuufikia uongofu hapa duniani.

Ijapokuwa kidhahiri matamshi ya aya hizi wapenzi wasomaji yanaonekana kumhutubu Bwana Mtume, lakini ni wazi kwamba si yeye anayesemezwa hapa, kwa sababu ni jambo lililo muhali na lisiloingia akilini kwamba Bwana Mtume awe na shaka na wahyi alioteremshiwa na Mola wake.

Hivyo anaowahutubu Allah katika aya hii ni mushirikina na Ahlul Kitab, lakini kama ilivyo katika aya nyingi za Quran lugha iliyotumika inaonyesha kuwa mhutubiwa ni bwana Mtume wakati kumbe mlengwa hasa ni watu wengine wa kawaida.

Pamoja na mambo mengine aya hizi zinatuelimisha kuwa shaka na hati hati ni vitu vya kawaida vinavyoweza kumtokea kila mtu. La muhimu ni kujivua na hali ya shaka kwa kurejea kwa maulamaa na wanazuoni wa kidini na kufikia kwenye daraja ya utambuzi kamili na yakini.

Funzo jengine tunalopata hapa ni kuwa endapo mtu ataendelea kubakia katika hali ya shaka na kutochukua hatua ya kuiondoa shaka aliyonayo si hasha akajikuta anaishia kwenye kukadhibisha na kuikataa moja kwa moja haki.

### AYA ZA 96 NA 97

Aya za 96 na 97 ndizo zinazotuhitimishia darsa yetu ya juma hili. Aya hizo zinasema:

إِنَّ الَّذِينَ حَقَّتْ عَلَيْهِمْ كَلِمَتُ رَبِّكَ لَا يُؤْمِنُونَ ﴿٩٦﴾

96. Hakika wale ambao neno la Mola wako limekwisha thibitika juu yao hawataamini.

وَلَوْ جَاءَتْهُمْ كُلُّ آيَةٍ حَتَّىٰ يَرَوُا الْعَذَابَ الْأَلِيمَ ﴿٩٧﴾

97. Ijapokuwa itawajia kila ishara mpaka waione adhabu inayoumiza.

Watu wamegawika makundi matatu katika suala la namna wanavyoamiliana na ukweli wa mafundisho ya dini.

Kundi la kwanza ni la wale wasioitambua haki na wala hawajishughulishi kutaka kuijua.

La pili ni la wale ambao haki hawaijui lakini wanaamua kufanya juhudi za kuitafuta hadi kuifikia. Ama kundi la tatu ni la wale ambao wameitambua haki lakini kwa kuwa inagongana na maslahi yao ya kimaada ya hapa duniani, hawako tayari kuifuata.

Aya tulizosoma zinawalenga watu wa kundi hili la tatu ambao nyoyo zao zimepiga weusi na kufanya kutu kutokana na inadi na ukaidi wao na ambao hakuna tena matumaini ya nyoyo zao kubadilika na kuiamini haki. Watu wa aina hii huwa ni katika wale walioghadhibikiwa na Mwenyezi Mungu; kwani hawawi tayari kuamini na kujisalimisha kwa Mola wao kama haijafikia hatua ya kuiona adhabu ya Mwenyezi Mungu kwa macho yao.

Tatizo la watu hao si kutopewa hoja za kiakili wala kutoonyeshwa muujiza, ambao hata kama wataonyeshwa pia hawatouamini. Tatizo lao ni kwamba hawaa na matamanio yao ya nafsi hayawaruhusu kuungama kile ambacho wamepata utambuzi wake.

Hivyo kama tutaona watu wengi hawaiamini haki, hilo lisitufanye tukautilia shaka ukweli wa maneno ya Mitume na vitabu vya mbinguni walivyokuja navyo. Bali tuelewe kwamba kuna watu ambao nafsi zao zimekubuhu kwa maovu na kuharibika kimaanawi kiasi kwamba hakuna chochote kile cha kuweza kuwaathiri wakabadilika.

Watu hao ni mithili ya mpira ambao kama utautupa baharini hakuna hata moja la maji litakalopenya na kuingia ndani yake. Hali ambayo ni matokeo ya kuziba kwa mpira tu vinginevyo bahari iko pale pale na maji yake yako kwa ajili ya kila mtu.

Baadhi ya nukta za kuzingatiwa katika aya hizi ni kuwa tusiwe na matumaini kwamba watu wote wataiamini haki, bali tujue kwamba maovu na madhambi ni mambo yanayofanya utandu juu ya moyo wa mtu unaomfanya asiwe tayari kuikubali haki.

Nukta nyingine ya kuzingatiwa katika aya hizi ni kuwa iko siku hata wale waliotopea katika kukadhibisha haki watabaini hakika hiyo lakini wakati huo watakuwa wamechelewa na kuikubali kwao haki wakati huo hakutowasaidia kitu.

Darsa ya 323 imeifikia tamati. Tunamwomba Allah atuonyeshe haki na kutuwafikisha kuifuata na atuonyeshe batili na kutupa taufiki ya kuiepuka. Amin.

Wassalaamu Alaykum Warahmatullahi Wabarakaatuh

## YUNUS 98-100

Assalaamu Alaykum Warahmatullahi Wabarakaatuh. Karibuni katika mfululizo mwingine wa darsa ya quran.

### AYA YA 98

Hii ni darsa ya 324, na tukiwa tunaendelea kuizungumzia sura ya 10 ya Yunus, tunaianza darsa yetu kwa aya ya 98 ambayo inasema:

فَلَوْلَا كَانَتْ قَرْيَةٌ آمَنَتْ فَنَفَعَهَا إِيمَانُهَا إِلَّا قَوْمَ يُونُسَ لَمَّا آمَنُوا كَشَفْنَا عَنْهُمْ عَذَابَ الْخِزْيِ فِي الْحَيَاةِ الدُّنْيَا وَمَتَّعْنَاهُمْ إِلَىٰ حِينٍ ﴿٩٨﴾

98. Kwa nini usiwepo mji mmoja ukaamini na imani yake ikawafaa isipokuwa kaumu Yunus? Waliamini na sisi tukawaondolea adhabu ya hizaya katika maisha ya dunia, na tukawasterehesha kwa muda.

Kama ambavyo tumewahi kuashiria katika darsa zetu za huko nyuma, ni kwamba utaratibu aliojiwekea Allah s.w.t kuhusiana na waja wake ni kuwapa fursa na muhula wa kutubia madhambi yao na kutenda amali njema ili kufidia waliyoyatanguliza huko nyuma.

Lakini pia kama tulivyowahi kueleza ni kwamba mlango wa toba uko wazi madamu mtu bado hajafikia lahadha ya kufikwa na mauti au kuteremkiwa na adhabu ya Mwenyezi Mungu.

Kwani kutubia katika lahadha mbili hizo au kuiamini haki katika wakati huo hakuwi na faida yoyote kwa mtu, na sababu ni kwamba imani na toba ya lahadha hizo hutokana na khofu ya mauti na adhabu na si kwa hiyari yake mtu.

Suala hilo la fursa na muhula wa kutubia na kuiamini haki hauishii kwa mtu binafsi tu, bali Allah ameuweka pia kwa kaumu na umma mzima wa watu. Kwa upande wa kaumu, ni ile ya Nabii Yunus tu (a.s) ndiyo ambayo watu wake walipoiona adhabu waliiamini haki na kujisalimisha kwa Mwenyezi Mungu, naye Mola Mrehemevu akaikubali imani yao na kuwapa fursa nyingine.

Historia inasimulia kwamba baada ya miaka mingi ya kazi ya tablighi aliyoifanya Nabii Yunus (a.s) kuwalingania watu wake lailaha illa llah ni watu wawili tu ndiyo walioukubali wito wa uongofu.

Akiwa katika siku za mwisho za uhai wake, na kutokana na kukata tamaa kwa watu wake kuiamini haki, Mtume huyo wa Allah aliwaapiza watu wa kaumu yake na kisha akaamua kuondoka na kwenda zake.

Kama ilivyo kawaida ni kwamba dua za Mitume huwa hazirudi, na kwa hivyo ilipasa watu wa kaumu yake wateremkiwe na adhabu.

Hata hivyo mtu mmoja mtambuzi na mwenye hekima kati ya wale wawili waliomuamini Mtume huyo alipoona Nabii Yunus ameshatoa tamko la kuwaapiza watu wake waliokataa kuamini haki aliwaendea watu hao na kuwaambia: "Sasa subirini mshukiwe na adhabu ya Mwenyezi Mungu, la kama mnataka mpate rehma zake Mola basi tokeni nje ya mji, na mutenganishe baina yenu na watoto wenu wadogo ili sauti za vilio vya watoto na za maombolezo ya mama zao waliotenganishwa nao ziweze kupanda na kusikika, na nyote pamoja mtubie kwa mliyoyafanya huko nyuma na kumwomba maghufira Allah s.w.t

Asaa kwa njia hiyo mkaweza kusamehewa. Hivyo watu hao wakaufuata wasia huo na hivyo adhabu haikuteremshwa tena, naye Nabii Yunus akarejea kwa watu wake.

Baadhi ya mafunzo tunayopata kutokana na ayah ii ni kuwa miongoni mwa kaumu zilizopita, ni kaumu ya Yunus tu ndiyo iliyotubia kwa wakati na kabla ya kushuka adhabu na toba yao ikapokelewa na kuamini kwao kukakubaliwa.

Funzo jengine tunalopata katika ayah ii ni kwamba hatima na majaaliwa ya watu yako mikononi mwao wenyewe, na hivyo kwa kuomba dua na kushtakia waja hali zao hiyo inaweza ikawa sababu ya kuzuia balaa lisiwashukie na rehma za Mola ziwamiminikie.

### AYA YA 99

Tunaiendeleza darsa yetu kwa aya ya 99 ambayo inasema:

وَلَوْ شَاءَ رَبُّكَ لَآمَنَ مَن فِي الْأَرْضِ كُلُّهُمْ جَمِيعًا أَفَأَنتَ تُكْرِهُ النَّاسَ حَتَّىٰ يَكُونُوا مُؤْمِنِينَ

﴿٩٩﴾

99. Angelitaka Mola wako wangeliamini wote waliomo katika ardhi. Je wewe utawalazimisha watu kwa nguvu mpaka wawe waumini?.

Moja ya kati ya mambo ambayo Mwenyezi Mungu sw amejifunga nayo mwenyewe ni kuwafikishia waja wake uongofu. Hata hivyo Mola Mwenye hikima hakutaka watu waiamini haki kwa nguvu na kulazimishwa.

Bali ametaka waamue kwa hiyari yao waja, ima kuiamini au kuikufuru haki. Tabaan baada ya kuchagua kwa hiyari yake mtu ima kuamini au kukufuru ajiweke tayari pia kwa jaza na malipo atakayopata kutokana na chaguo lake.

Kwa kuzingatia kwamba sifa moja kubwa ya Bwana Mtume Muhammad **(s.a.w.w)** kama ilivyoelezwa na quran ni kwamba alikuwa na hamu kubwa ya kuona watu wa umati wake wanaiamini haki na akiumia na kuungulika mno kwa kuwaona wamezama katika dimbwi la upotofu, lakini kwa kuwa Allah s.w.t ametaka imani ya waja itokane na hiyari yao hivyo anamhutubu Mtume wake kwa kumwambia kwamba pamoja na hamu kubwa uliyonayo usifikirie kuwafanya watu waumini hata kwa kuwateza nguvu, kwani lau Mola wako angetaka iwe hivyo wanaadamu wote wangeiamini haki.

Moja ya nukta za kuzingatiwa katika ayah ii ni kuwa imani huwa na thamani inapotokana na hiyari ya mtu, ama ikiwa itatokana na kulazimishwa haiwezi kuwa na faida kwa mtu.

### AYA YA 100

Darsa ya 324 inahitimishwa na aya ya 100 ambayo inasema:

وَمَا كَانَ لِنَفْسٍ أَن تُؤْمِنَ إِلَّا بِإِذْنِ اللَّـهِ ۚ وَيَجْعَلُ الرِّجْسَ عَلَى الَّذِينَ لَا يَعْقِلُونَ ﴿١٠٠﴾

100. Na hawezi mtu kuamini ila kwa idhini ya Mwenyezi Mungu. Naye hujaalia adhabu iwafike wasiotumia akili zao.

Kama tujuavyo, watu hawalazimishwi kuiamini haki, na kuamini kwa kulazimishwa hakuna thamani yoyote.

Pamoja na hayo ni taufiki ya Mola ndiyo inayoufanya moyo wa mtu uikubali na kuiamini haki kwa hiyari na ukunjufu. Kwani ni yeye ndiye anayetukamilishia suhula zote kuanzia za kutufikia uongofu wenyewe kupitia kwa Mitume wake, pamoja na kutupa akili timamu ya kuchanganua na kupambanua zuri na baya, la kheri na la shari na lile la kimantiki na lisiloingia akilini.

Hivyo mtu asije akaingiwa na ghururi na kumpitikia kwamba ni uhodari wake ndio uliomfanya kuitambua haki na kuifuata. Na kwa hakika kila mtu anapojiona amepata taufiki ya kushikamana barabara na kamba ya uongofu, basi amshukuru sana Mola wake na kuomba taufiki ya kudumu katika kushikamana na mambo ya kheri. Amin.

Wassalaamu Alaykum Warahmatullahi Wabarakaatuh.

9

# TAFSIRI YA SUURAT YUUNUS

## YUNUS 93-97

Bismillahir Rahmanir Rahim. Assalaamu Alaykum Warahmatullahi Wabarakaatuh.

Tunamshukuru Mwenyezi Mungu mtukufu kwa kutuwafikisha kukutana tena katika darsa yetu hii.

### AYA YA 101

Sura ya 10 ya Yunus ndiyo tunayoizungumzia kwa sasa, na hii ni darsa ya 325 tunayoianza kwa aya ya 101 ambayo inasema:

قُلِ انظُرُوا مَاذَا فِي السَّمَاوَاتِ وَالْأَرْضِ ۚ وَمَا تُغْنِي الْآيَاتُ وَالنُّذُرُ عَن قَوْمٍ لَّا يُؤْمِنُونَ ﴿١٠١﴾

101. Sema: Angalieni yaliyomo mbinguni na kwenye ardhi! Na ishara zote na maonyo hayawafai kitu watu wasioamini.

Katika aya zilizotangulia tulisema kuwa kutotumia watu akili zao na kutotafakari juu ya alama na ishara za uwezo wa Allah ndiyo sababu ya watu kukufuru na kuikana haki.

Aya tuliyosoma inatilia mkazo suala la kutadabari na kubainisha kuwa, kutafakari na kuzingatia kwa kina madhihirisho ya uumbaji wa Allah ni utangulizi wa kumfikisha mtu kwenye imani thabiti na sahihi.

Kwa upande mwingine kama tulivyosisitiza katika darsa iliyopita na nyingine kadhaa, imani lazima itokane na hiyari ya mtu na si kwa kulazimishwa na kutezwa nguvu, na ndiyo maana aya hii ya 101 inasisitiza juu ya kutafakari ili kwa kupitia njia hiyo ya uelewa na ufahamu mtu aiamini haki na kuweza kudumu na imani aliyonayo.

Bila shaka utafiti sahihi na wa kutafuta ukweli juu ya chungu ya maajabu yaliyomo katika mbingu na ardhi na ulimwengu mzima wa uumbaji humfanya mwanaadamu atambue adhama ya Mola wake na hivyo kunyenyekea na kujisalimisha kwa Muumba asiye na mshirika.

Pamoja na hayo bado wanakuwepo watu ambao licha ya kushuhudia ishara za adhama ya Mola Muumba huamua kuikana na kuikataa haki. Baadhi ya mafunzo tunayopata kutokana na aya hii ni kuwa kutafakari na kutadabari juu ya uumbaji ni njia inayoweza kutumiwa na kila mtu kwa ajili ya kumjua Mwenyezi Mungu.

### AYA YA 102

Ifuatayo sasa ni aya ya 102 ambayo inasema:

فَهَلْ يَنتَظِرُونَ إِلَّا مِثْلَ أَيَّامِ الَّذِينَ خَلَوْا مِن قَبْلِهِمْ ۚ قُلْ فَانتَظِرُوا إِنِّي مَعَكُم مِّنَ الْمُنتَظِرِينَ ﴿١٠٢﴾

102. Basi je wanagojea jingine ila kama yaliyotokea siku za watu waliopita kabla yao? Sema: Basi ngojeni! Nami ni pamoja nanyi katika wanaongojea.

Katika aya zilizotangulia Mwenyezi Mungu amewataka wapinzani wa haki kutafakari na kuzingatia kwa makini ishara za kuwepo Muumba wa ulimwengu katika mbingu na ardhini.

Aya tuliyosoma hivi punde inasema wale ambao hawako tayari kutafakari juu ya hayo basi wajiweke tayari kukabili siku ngumu za mashaka na adhabu. Kwani utaratibu aliouweka Allah kuhusiana na uma au jamii za watu mbali mbali ni kwamba kama ilivyo kwa watu mmoja mmoja, majaaliwa na hatima ya jamii nzima ya watu hutegemea mwenendo wa akthari ya watu walioko katika jamii hiyo.

Kama wengi wao watakuwa ni watu wema basi jamii nzima huwa na muelekeo wa kutengenea hata kama watu wachache kati yao watakuwa mafasiki; la kama wengi wao watakuwa ni waovu basi jamii nzima itatumubukia kwenye ufisadi na kupatwa na mwisho mbaya hata kama ndani yake baadhi ya watu watakuwa ni waja wema.

Historia ya kaumu zilizopita kama zile za Manabii Nuh, Lut na Hud as ni uthibitisho juu ya kutobadilika kwa utaratibu huo wa Allah s.w.t Hivyo bwana Mtume anatakiwa na Mola awaeleze Mushirikina wa Makka kwamba kama nao pai wataamua kusimama dhidi ya risala ya haki watafikwa na hatima sawa na iliyowapata watu wan kaumu hizo.

Miongoni mwa mafunzo tunayoyapata kutokana na aya hii ni kuwa ni historia ya waliotangulia ni funzo na ibra kwa wanaofuatia.

### AYA YA 103

Ifuatayo sasa ni aya ya 103 ambayo inasema:

ثُمَّ نُنَجِّي رُسُلَنَا وَالَّذِينَ آمَنُوا ۚ كَذَٰلِكَ حَقًّا عَلَيْنَا نُنجِ الْمُؤْمِنِينَ ﴿١٠٣﴾

103. Kisha sisi huwaokoa Mitume wetu na walioamini. Ndio kama hivyo, inatustahiki kuwaokoa Waumini.

Ikiendeleza yale yaliyokuja katika aya iliyotangulia kuhusiana na watu kupatwa na adhabu ya papa hapa duniani, aya ya 103 ya suratu Yunus inasema kwa kuwa hailaiki katika uadilifu wa Allah kuwachanganya wema na wabaya katika adhabu, hivyo kila kaumu inayofkia hatua ya kustahiki kufikwa na adhabu ni wale walio waovu na wale waliokuwa hawayajali maovu yanayotendeka katika jamii ndio wanakaopatwa na adhabu ya Allah, ama wale walio waumini Mwenyezi Mungu atawaokoa na adhabu hiyo.

Baadhi ya nukta za kuzingatiwa katika aya hii ni kuwa wale walio waumini wa kweli Mwenyezi Mungu huwalinda na adhabu hata ya hapa duniani, japokuwa watakuwa wakiishi katika jamii ya watu mafasiki.

### AYA YA 104

Ifuatayo sasa ni aya ya 104 ambayo inasema:

قُلْ يَا أَيُّهَا النَّاسُ إِن كُنتُمْ فِي شَكٍّ مِّن دِينِي فَلَا أَعْبُدُ الَّذِينَ تَعْبُدُونَ مِن دُونِ اللَّـهِ وَلَـٰكِنْ أَعْبُدُ اللَّـهَ الَّذِي يَتَوَفَّاكُمْ ۖ وَأُمِرْتُ أَنْ أَكُونَ مِنَ الْمُؤْمِنِينَ ﴿١٠٤﴾

104. Sema: Enyi watu ikiwa nyinyi mnayo shaka katika dini yangu basi mimi siwaabudu mnaowaabudu nyinyi badala ya Mwenyezi Mungu. Lakini mimi ninamwabudu Mwenyezi Mungu anayekufisheni. Na nimeamrishwa niwe miongoni mwa Waumini.

Baada ya aya ziliowahutubu washirikina na kuwabainishia ipi itakuwa hatima yao, aya hii inamtaka Bwana Mtume awaambie watu hao kuwa kama wanadhani kwamba wewe utayumba na kutia shaka katika kufuata njia yako ya haki na pengine kukushawishi ulegeze msimamo katika itikadi yako basi wape jibu zito na la wazi kwamba hutomwabudu mwingine yeyote ghairi ya

Mola wako Allah s.w.t na katu hutoyatukuza msanamu yao hayo wanayoyaabudu. Waambie kwamba mimi ninamwabudu Mungu ambaye mauti yangu na yenu yako mikononi mwake na hamuwezi nyinyi abadani kuyakwepa hayo wala hayo masanamu yenu pia hayana uwezo wa kukuepusheni na kifo.

Baadhi ya mafunzo tunayopata kutokana na aya hii ni kuwa shaka inayotiwa na wengine juu ya haki hata kama watakuwa wengi namna gani isituyumbishe katika kufuata njia ya uongofu.

Aidha aya inatuonyesha kuwa aliye na ustahiki wa kuabudiwa ni yule ambaye uhai wetu na mauti yetu yako mikononi mwake.

### AYA ZA 105 NA 106

Darsa ya 325 inahitimishwa na aya za 105 na 106 ambazo zinasema:

وَأَنْ أَقِمْ وَجْهَكَ لِلدِّينِ حَنِيفًا وَلَا تَكُونَنَّ مِنَ الْمُشْرِكِينَ ﴿١٠٥﴾

105. Na uelekeze uso wako kwenye dini ya kweli wala usiwe katika washirikina.

وَلَا تَدْعُ مِن دُونِ اللَّهِ مَا لَا يَنفَعُكَ وَلَا يَضُرُّكَ ۖ فَإِن فَعَلْتَ فَإِنَّكَ إِذًا مِّنَ الظَّالِمِينَ ﴿١٠٦﴾

106. Na wala usiwaombe wasiokuwa Mwenyezi Mungu ambao hawakufai kitu wala hawakudhuru. Ukifanya hivyo basi utakuwa miongoni mwa waliodhulumu.

Katika kuwatangazia watu na hasa washirikina yale aliyoamriwa na Mola wake, Bwana Mtume anabainisha katika aya hizi kuwa ni wajibu kuifuata na kushikamana nayo njia iliyonyooka na kuepuka kila aina ya upotofu. Ama kinyume chake, itikadi ya mushirkina imejaa upotofu na mambo ya uzushi chungu nzima na muhimu zaidi ni kuwa hivyo vinavyoabudiwa na washirikina hao yaani masanamu, havina uwezo wa kumdhuru wala kumnufaisha mtu kwa lolote.

Hivyo anayevielekea na kuviabudu vitu hivyo huwa ameidhulumu nafsi yake na pia kuifanyia dhulma dini ya haki ya mbinguni.

Baadhi ya mafunzo tunayopata kutokana na aya hizi ni kuwa dini ya kufuata ni ile inayokubaliana na maumbile ya mwanadamu. Aidha aya zinatuonyesha kuwa kila mwenye akili na busara hufanya kitu ambacho ima kitamletea manufaa au kumuepusha na madhara.

Lakini kama tujuavyo masanamu na miungu wengine wengine wote bandia hawana uwezo wa hayo.

Kwa haya machache basi tunaifunga darsa yetu hii kwa kumwomba Allah atulinde na kila aina ya shirki na kutuwafikisha kumwabudu yeye kwa ikhlasi. Amin.

Wassalaamu Alaykum Warahmatullahi Wabarakaatuh.

## YUNUS 107-109

Assalaamu Alaykum Warahmatullahi Wabarakaatuh.

Tunamshukuru Mwenyezi Mungu mtukufu kwa kutuwafikisha kukutana tena katika darsa yetu hii.

### AYA YA 107

Sura ya 10 ya Yunus ndiyo tunayoizungumzia kwa sasa, na hii ni darsa ya 326 na ya mwisho inayozungumzia sura hiyo tunayoianza kwa aya ya 107 ambayo inasema:

وَإِن يَمْسَسْكَ اللَّـهُ بِضُرٍّ فَلَا كَاشِفَ لَهُ إِلَّا هُوَ ۖ وَإِن يُرِدْكَ بِخَيْرٍ فَلَا رَادَّ لِفَضْلِهِ ۚ يُصِيبُ بِهِ مَن يَشَاءُ مِنْ عِبَادِهِ ۚ وَهُوَ الْغَفُورُ الرَّحِيمُ ﴿١٠٧﴾

107. Na kama Mwenyezi Mungu akikugusisha dhara, basi hapana wa kukuondolea ila yeye. Na akikutakia kheri basi hapana awezaye kurudisha fadhila zake. Huzifikisha kwa amtakaye katika waja wake. Naye ni Mwingi wa Kusamehe na Mwingi wa Kurehemu.

Katika aya ya mwisho tuliyoisoma katika darsa iliyopita Allah s.w.t alimtaka Bwana Mtume Muhammad **(s.a.w.w)** asimame imara na kuwatangazia kinagaubaga washirikina kuwa njia yake yeye ni ya tauhidi, na wala hatolegeza msimamo kwa sababu ya kuwavutia ao washirikina waukubali Uislamu.

Aya tuliyosoma inaendeleza yale yaliyokuja katika aya iliyotangulia na kumwambia Bwana Mtume na Waislamu kwa jumla kwamba, elewa kuwa kheri yoyote utakayopata au dhara yoyote itakayofika iko mikononi mwa Mola wako Allah s.w.t, na hakuna yeyote ghairi ya yeye aliye na uwezo wa kukupa kheri au kukupokonya neema yoyote uliyopewa na yeye Mola. Kama ambavyo bila ya ridhaa yake Mola, hakuna mtu yeyote awezaye kukudhuru, kama ambavyo endapo Mwenyezi Mungu s.w.t atataka dhara yoyote ile impate mja hakuna yeyote aliye na uwezo wa kumkinga mja na dhara hiyo.

Baadhi ya mafunzo tunayopata kutokana na aya hii ni kuwa mushirikina na makafiri waelewe kwamba kukataa kwao kuiamini haki hakutawawezesha kutoka nje ya irada ya Allah s.w.t, na kwa hakika kile alichoandika Mola kiwafike ndicho kitakachotokea. Aidha aya inatuelimisha kuwa kheri na neema azipatazo mja zinatokana na ihsani na fadhila zake Mola na wala si kwa kustahiki mja.

## AYA YA 108

Ifuatayo sasa ni aya ya 108 ambayo inasema:

قُلْ يَا أَيُّهَا النَّاسُ قَدْ جَاءَكُمُ الْحَقُّ مِن رَّبِّكُمْ ۖ فَمَنِ اهْتَدَىٰ فَإِنَّمَا يَهْتَدِي لِنَفْسِهِ ۖ وَمَن ضَلَّ فَإِنَّمَا يَضِلُّ عَلَيْهَا ۖ وَمَا أَنَا عَلَيْكُم بِوَكِيلٍ ﴿١٠٨﴾

108. Sema: Enyi watu haki imekwisha kukujieni kutoka kwa Mola wenu. Basi anayeongoka, anaongoka kwa faida ya nafsi yake, na anayepotea, anapotea kwa khasara ya nafsi yake. Na mimi si mlinzi juu yenu.

Katika aya hii ambayo ni moja kabla ya aya ya mwisho ya suratu Yunus Bwana Mtume Muhammad **(s.a.w.w)** anawahutubu watu wote kwa jumla kwamba mimi nina jukumu la kukufikishieni wito wa wahyi wa Mola wangu na kukulinganieni kuifuata njia yake tu; na wala sina haki ya kukulazimisheni muukubali wito huo.

Kila mmoja kati yenu anaweza kuamua kwa hiyari yake kuukubali uongofu na kuongoka, au kuukana na kupotoka. Lakini jueni kwamba kuamini kwenu na kukufuru kwenu hakuna tofauti yoyote kwa Mwenyezi Mungu s.w.t wala mimi Mtume wake, na kwa hakika kama ni kupata faida au madhara na hasara, hilo litakurudieni nyinyi wenyewe.

Kwani Mwenyezi Mungu yeye ni mkwasi wala hahitaji chohcote kwenu, nami pia nimetimiza wajibu wangu wa kukulinganieni na kukufikisheni

risala ya uongofu kutoka kwa Mola wenu, na hivyo sina dhima yoyote juu ya kuamini au kutoamini kwenu.

Baadhi ya nukta za kuzingatiwa katika aya hii ni kuwa Mwenyezi Mungu ameondoa dhima kwa waja wake kwa kuwaonyesha na kuwabainisha njia ya haki. Kufuata au kutofuata hilo liko katika hiyari ya waja wenyewe.

Nukta nyengine ya kuzingatiwa katika aya hii ni kuwa jukumu la maulamaa na wale wafanyao tablighi ya dini ni kuwaelimisha na kuwaonyesha njia watu na si kuwalazimisha waikubali na kuifuata.

### AYA YA 109

Darsa ya 326 na sura yetu ya Yunus inahitimishwa na aya ya 109 ambayo inasema:

وَاتَّبِعْ مَا يُوحَىٰ إِلَيْكَ وَاصْبِرْ حَتَّىٰ يَحْكُمَ اللَّهُ وَهُوَ خَيْرُ الْحَاكِمِينَ ﴿١٠٩﴾

109. Na (nimeambiwa): Fuata yanayofunuliwa kwako kwa Wahyi. Na vumilia mpaka Mwenyezi Mungu ahukumu, na yeye ndiye mbora wa mahakimu.

Aya hii ya mwisho ya sura hii inasisitiza kwa mara nyingine juu ya kushikamana barabara na njia ya haki ya risala ya wahyi utokao kwa Mola Muumba, kwanza kabisa ikimuelekea bwana Mtume mwenyewe na kisha waumini kwa jumla, kwa kuwataka waendelee kuwa na subra hadi ushindi wa haki dhidi ya batili.

Kama inavyojulikana mataghuti na madhalimu hufanya kila vitimbi na njama ili kuwakwamisha waumini wa kweli wasiweze kushikamana na kamba ya lailaha illa llah kama inavyostahiki.

Na ndiyo maana aya inawataka waumini kusimama kidete dhidi ya njama hizo na kuvumilia tabu na mashaka yote yatakayowapata katika njia hiyo. Alaa kulli haal Mwenyezi Mungu s.w.t anaona kila kinachofanywa na waja wake wote, na siku itafika ambapo atahukumu baina yao kwa uadilifu. Lakini hata hapa duniani pia, pale waumini wanaposimama kidete kukabiliana na madhalimu, mwishowe hupata nusra ya Allah na haki kuishinda batili. Baadhi ya mafunzo tunayopata kutokana na aya hii ni kuwa watu wana hiyari ama kuamini au kukufuru, hata hivyo kukufuru kwao kusitufanye sisi tukaingiwa na shaka katika kufuata njia ya uongofu ya kushikamana na maamrisho ya Mola wetu na kujiweka mbali na makatazo yake. Wapenzi wasomaji.

darsa ya 326 imefikia tamati na kuhitmisha pia tarjumi na maelezo ya sura ya kumi ya Yunus.

Tunamwomba Mwenyezi Mungu atuwafikishe kuyatekeleza kivitendo yale yote tuliyojifunza ndani ya sura hii, Amin.

Wassalaamu Alaykum Warahmatullahi Wabarakaatuh.

### SHARTI YA KUCHAPA

Sharti ya kuchapa au kusambaza ni kutaja rejeo hili. haki zote zimehifadhiwa na Taasisi ya Al-Hasanain Taasisi ya Imamu Husein (a.s)

Site ya Al-Imaamaini Al-Hassanaini (a.s) ya usambazaji wa utamaduni wa Kiislamu na mafunzo ya Kidini.

### MWISHO WA TAFSIRI YA SUURAT YUUNUS

## YALIYOMO

**1** ........................................ **TAFSIRI YA SUURAT YUUNUS**
1 ........................................................ UTANGULIZI
1 ............................... MKUSANYAJI WA MAKALA HIZI NI:
1 ............................................ SALIM SAID AL-RAJIHIY
**2** ........................................ **TAFSIRI YA SUURAT YUUNUS**
2 ............................................. MWANZO WA MAKALA
2 ..................................... AYA YA KWANZA NA YA PILI
3 ......................................................... AYA YA TATU
3 ........................................................... AYA YA NNE
4 ................................................ SURAT YUNUS 5-10
4 ....................................................... AYA YA 5 NA 6
5 ............................................................ AYA 7 NA 8
5 ........................................................... AYA 9 NA 10
**7** ........................................ **TAFSIRI YA SUURAT YUUNUS**
7 ................................................ SURAT YUNUS 11-14
7 ............................................................ AYA YA 11
7 ............................................................ AYA YA 12
8 .................................................. AYA YA 13 NA 14
9 ................................................ SURAT YUNUS 15-18
9 ............................................................ AYA YA 15
9 .................................................. AYA ZA 16 NA 17
10 .......................................................... AYA YA 18
**12** ...................................... **TAFSIRI YA SUURAT YUUNUS**
12 .............................................. SURAT YUNUS 19-23
12 .......................................................... AYA YA 19
12 .......................................................... AYA YA 20
13 .......................................................... AYA YA 21
13 ................................................ AYA ZA 22 NA 23
14 .............................................. SURAT YUNUS 24-27
14 .......................................................... AYA YA 24
15 .......................................................... AYA YA 25
15 .......................................................... AYA YA 26
16 .......................................................... AYA YA 27
17 .............................................. SURAT YUNUS 28-33
17 ................................................ AYA ZA 28 NA 29

17 ........................................................ AYA YA 30
18 ........................................................ AYA YA 31
18 ................................................. AYA ZA 32 NA 33
19 ............................................... SURAT YUNUS 34-38
19 ................................................. AYA ZA 34 NA 35
20 ........................................................ AYA YA 36
20 ................................................. AYA ZA 37 NA 38
21 ............................................... SURAT YUNUS 39-44
21 ................................................. AYA ZA 39 NA 40
22 ........................................................ AYA YA 41
23 ............................................. AYA ZA 42, 43 NA 44
24 ............................................... SURAT YUNUS 45-49
24 ........................................................ AYA YA 45
24 ........................................................ AYA YA 46
25 ........................................................ AYA YA 47
25 ..............................................AYA ZA 48 NA NA 49
**27** ...................................... **TAFSIRI YA SUURAT YUUNUS**
27 ............................................... SURAT YUNUS 50-56
27 ................................................. AYA ZA 50 NA 51
27 ........................................................ AYA YA 52
28 ................................................. AYA ZA 53 NA 54
28 ................................................. AYA ZA 55 NA 56
29 ............................................... SURAT YUNUS 57-61
29 ................................................. AYA ZA 57 NA 58
30 ................................................. AYA ZA 59 NA 60
31 ........................................................ AYA YA 61
**32** ...................................... **TAFSIRI YA SUURAT YUUNUS**
32 .........................................................YUNUS 62-67
32 ................................................... ZA 62, 63 NA 64
33 ................................................. AYA ZA 65 NA 66
33 ........................................................ AYA YA 67
34 .........................................................YUNUS 68-73
34 ............................................. AYA ZA 68, 69 NA 70
35 ........................................................ AYA YA 71
36 ................................................. AYA ZA 72 NA 73
**37** ...................................... **TAFSIRI YA SUURAT YUUNUS**

37 ........ YUNUS 74-78
37 ........ AYA 74 NA 75
38 ........ AYA ZA 76 NA 77
38 ........ AYA YA 78
**40 ........ TAFSIRI YA SUURAT YUUNUS**
40 ........ YUNUS 79-86
40 ........ AYA ZA 79 NA 80
40 ........ AYA ZA 81 NA 82
41 ........ AYA YA 83
41 ........ AYA ZA 84, 85 NA 86
42 ........ YUNUS 87-92
42 ........ AYA YA 87
43 ........ AYA ZA 88 NA 89
44 ........ AYA ZA 90, 91 NA 92
**45 ........ TAFSIRI YA SUURAT YUUNUS**
45 ........ YUNUS 93-97
45 ........ AYA YA 93
45 ........ AYA ZA 94 NA 95
46 ........ AYA ZA 96 NA 97
47 ........ YUNUS 98-100
47 ........ AYA YA 98
48 ........ AYA YA 99
49 ........ AYA YA 100
**50 ........ TAFSIRI YA SUURAT YUUNUS**
50 ........ YUNUS 93-97
50 ........ AYA YA 101
50 ........ AYA YA 102
51 ........ AYA YA 103
51 ........ AYA YA 104
52 ........ AYA ZA 105 NA 106
52 ........ YUNUS 107-109
52 ........ AYA YA 107
53 ........ AYA YA 108
54 ........ AYA YA 109
54 ........ SHARTI YA KUCHAPA
54 ........ MWISHO WA TAFSIRI YA SUURAT YUUNUS

55 .......................................................... YALIYOMO